// CHUO KIKUU CHA NAIROBI

**IDARA YA KISWAHILI**

# UCHUNGUZI WA SITIARI DHANIFU KATIKA METHALI ZA KISWAHILI - MTAZAMO WA NADHARIA YA UHUSIANO

**MISHECK NKANGA GAICHU**

**C50/66914/2013**

**TASNIFU HII INAWASILISHWA KWA MINAJILI YA KUKIDHI MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2016**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu asili, haijawahi kuwasilishwa kwa ajili ya shahada yoyote katika chuo kingine. Hakuna anayeruhusiwa kuinakili bila ya idhini yangu au /na Chuo Kikuu cha Nairobi.

……………………………………………… ………………………………

MISHECK NKANGA GAICHU TAREHE

C50/66914/ 2013

MTAHINIWA

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa mzamili:

……………………………………………………… ……………………………..

**DKT. JAMES NYACHAE MICHIRA** **TAREHE**

MSIMAMIZI

………………………………………………………..... ………………………………

**DKT. HANNAH MWALIWA** **TAREHE**

MSIMAMIZI

JULAI 2016

## KUTABARUKU

Kwa familia yangu, bibi yangu Dorcas Muthoni na mtoto wangu Marx Mwenda, ninawapongeza kwa kuniombea na kunikumbusha kuwa ningali nazamili. Baraka za Mungu zimwandame kila wakati.

Ninawatabarukia wazazi wangu: Johana Gaichu Munyori na Jeniffer Karigu Gaichu. Asante kwa kunipa azimio la maisha, msingi bora wa elimu na motisha wa maisha ambao ni msingi wa ufanisi wangu wa leo.

Namtabarukia kasisi Fr. Jorge Alias wa kanisa la Katoliki la Dayosisi ya Meru kwa kuwa mfadhili wangu nikiwa Shule ya Upili ya Gatunga.

Ninawatabarukia ndugu zangu: Augustine, David, Geoffrey, Gideon, Daniel, Charity, Sabina, Japheth, Julia, Regina na Elizabeth kwa maombi yao.

Shukrani za kipekee zimwendee Bw. Peter Mugwika- binamu yangu wa kipekee mwenye busara sawa na Suleiman- kwa kunipa moyo wa kustahimili na ari ya kuvumilia wakati nilipolemewa. Mungu ambariki.

Mbarikiwe.

Asante na baraka za Mungu zimwandame maishani.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa, ninamshukuru Mungu kwa kunipa afya, uwezo na nguvu za kuendeleza masomo yangu bila vikwazo vyovyote.

Pili, ninawashukuru wazazi wangu, kwa malezi bora, upendo, uelekezi na ushauri mkubwa waliokuwa wakinipa kila wakati tukiwa nao pamoja na maombi yao ambayo yalinisaidia kuendelea na kazi hii.

Shukrani za kipekee ziwaendee wasimamizi wangu - Dkt. Hannah Mwaliwa na Dkt. Michira Nyachae - kwa kujitwika jukumu kali la kuishughulikia kazi hii ambayo ilihitaji subira na kujitolea kwingi, aidha, kwa kunipa mwongozo wa kiakademia- kwa hekima kubwa- wakati nilipokuwa nikiandika tasnifu hii.

Shukrani zangu pia ziwafikie wakuu mbalimbali wa idara ya Kiswahili- Profesa Hamu Habwe, Profesa Kinene wa Mutiso, Profesa Rayya Timmamy, Dkt. Iribe Mwangi, Dkt. Ayub Mukhwana, Dkt. Jefwa G. Mweri, Dkt. Amiri Swaleh, Bw. Mungania- kwa kunifunza katika kiwango cha uzamili, kunipa ujuzi na uwezo wa kuelewa kutumia lugha ya Kiswahili.

Shukrani zangu ziwafikia wanafunzi wenzangu: Bwana Mutali, Kimetto, Kihara, Kevin, Mosota, Agnes, Nduku, Adeline, Nyutu, Mengisto, Asha, Magdalene, Zahr, Xariun, Bosco, Mwangi, Caroline, Asiko, Polycap, Mogusu, Bosibori, Norah na Wanjiru kwa kunipa matumaini na kukubali kufanya kazi pamoja nami tukiwa darasani. Kutangamana kwangu nao kumechangia kupata nililokusudia maishani mwangu.

# IKSIRI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza lugha kama inavyotumiwa katika methali za sitiari za Kiswahili. Methali za kisitiari zimebainisha kuwa maana halisi ya neno inaweza kubadilika na kuchukua maana nyingine ambayo ni tofauti na maana ya kiisimu ya neno husika. Utafiti huu ulilenga kuchunguza umbo la kileksika na kuchunguza namna muktadha limamotumika neno huweza kubadilisha maana halisi ya neno lililotumika kama sitiari katika methali za sitiari. Matokeo ya utafiti huu yamethibitisha kuwa maana halisi ya leksimu hubadilika na maana mpya huafikiwa kulingana na kanuni ya mawasiliano, kanuni tambuzi pamoja na muktadha ambapo neno hutokea. Huhamishaji huu- wa maana- hupatikana baada ya kuwezesha vitomeo vya kiensaiklopedia ambavyo husababisha upanuaji wa dhana husika. Katika utafiti huu tulishughulikia usuli wa mada, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, haipothesia, upeo na mipaka ya utafiti, sababu ya kuchagua mada, yaliyoandikwa kuhusu mada, msingi ya kinadharia, na mbinu za utafiti. Aidha, tumeshughulikia historia na maendeleo ya ufasiri wa sitiari na uainishaji wa methali na sitiari: kulingana na maoni ya wataalamu kama vile: Sperber na Wilson, Lakoff na Johnson na Shelestiuk. Sifa na femomena za jumla zinazopatikana katika sitiari za methali za Kiswahili. Mwisho, tumechanganua leksimu zinazopatikana katika methali za Kiswahili kutoka kwa methali teule na kuonyesha namna maana ya neno- lililotumiwa kisitiari-huafikiwa kulingana na muktadha ilichunguzwa. Baadaye tumeotoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya kile tulichoshughulikia katika utafiti huu. Aidha, mapendekezo ya yale yanayofaa kuchunguzwa katika siku za baadaye pia yalitolewa.

## FAFANUZI ZA DHANA NA/ISTILAHI MUHIMU KAMA ZILIVYOTUMIKA KATIKA UTAFITI HUU

**Athari za kimuktadha** Ni aina za athari za kiisimu ambazo hutambua mchango wa muktadha katika kufasiriwa kwa kipashio cha kiisimu.

**Dhana ya sifa maalum ya kihali (*ad-hoc*)** Ni dhana maalum inayozuka kulingana na kihali ambayo neno limetumika. Ina misingi yake katika ufasiri wa dhana, jumbe za kimuktadha na matarajio ya kipragmatiki. (Cartson 2007).

**Dhana kisitiari** Ni picha ya akilini inayojengwa na majina, maelezo ambayo hupewa mtu au kitu, kwa kawaida mtu au kitu hakiwezi kuwa hivyo.

**Dhana msingi** Ni dhana ambayo inapewa sifa za dhana ingine. Mfano Upishi kupewa sifa za kuni.

**Eksiplekecha** Ni maana wazi inayoendelezwa na umbo la kiisimu lililosimbwa. Maana hii hutokea tamko katika umbo la mantiki.

**Elementi/ fenomena** Sehemu ya kitu kizima ambayo inaweza kutambuliwa kama sifa katika uchunguzi.

**Implekecha** Ni umbo mantiki linalotokana na uwezeshaji wa maana kimuktadha.

**Kipashio cha kiisimu/lugha** Ni kipashio asilia ambacho kupitia kwacho, jumbe za kiisimu huchanganuliwa.

**Leksimu-** Ni kipashio cha msingi cha lugha chenye maana kama vile neno, mzizi, nahau. Hutumika kiisimu kerejelea neno lililo na maana bainifu na lenye kuambatanishwa na dhana za kitamaduni. Inaweza kuwa na miundo mbalimbali.

**Maana hamishwa** Ni matumizi ya neno kistiari.

**Methali za sitiari** Ni methali zilizo na muundo wa ulinganisho wa dhana kwa njia ya moja kwa moja.

**Muktadha** Ni sauti, neno, au kishazi kinachotangulia au kufuata kipashio fulani cha kiisimu katika tamko au matini.

Ni sifa za mazingira ya ulimwengu halisi ambapo usemi hupata maana. Katika utafiti huu tutaangalia muktadha kama mazingira halisi ya kutumia usemi.

**Nomino dhahania** Ni nomino ambazo zinataja vitu vya kidhanifu kama vile: furaha, ushujaa, upweke, ukweli na majina mengineyo ya sampuli hii. Kinachorejewa hakiwezi kuonekana bayana.

**Paremiolojia** Taaluma inayojishughulisha na uchunguzi wa methali.

**Pragmatiki leksika-** Tawi la kiisimu linalofafanua namna maana ya dhana inavyowasilishwa na namna dhana inavyoweza kubadilika kimaana kulingana na muktadha.

**Semantiki leksika -** Ni semantiki inayolenga kuchunguza uhusiano baina ya neno na dhana inayosimbwa.

**Sitiari** Ni tamathali ya lugha ambayo neno au kishazi huweza kupewa au kutajia mtu au kitu ambacho katika hali ya kawaida hakiwezekani kiwe kama kinavyotajwa.

**Sitiari dhanifu** Ni sitiari au ulinganifu wa kitamathali ambapo wazo au dhana moja ueleweka kwa msingi ya dhana/wazo lingine.

**Upanuzi wa kikategoria -** Ni neno linalotumiwa kwa msingi ya upanuzi kumaanisha kitu kingine kama vile kutumia neno la mtu au maneno ya kawaida kurejelea kategoria pana.

## YALIYOMO


**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ……..………………………………….1**

1.1 Usuli wa mada……………………………………………………………..1

1.2 Tatizo la utafiti……………………………………………………………4

1.3 Madhumini ya utafiti………………………………………………........... 4

1.4 Nadharia tete…………………………………………………….……… 4

1.5 Sababu ya kuchagua mada……………………………………………….. 5

1.6 Upeo na mipaka ya utafiti ………………………………………..………… 6

1.7 Yaliyoandikwa huhusu mada……………………………………………….. 7

1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu methali……………………………………. 7

1.7.2 Yaliyoandikwa kuhusu sitiari…………………………………… 7

1.7.3 Yaliyoandikwa kuhusu Nadharia ya Uhusiano……………………. 9

1.8 Msingi wa kinadharia……………………………………………………. 11

1.8.0 Madai ya Nadharia ya Uhusiano…………………………….......... 12

1.8.1 Kanuni za Nadharia ya Uhusiano………………………………… 13

1.8.1.1 Kanuni tambuzi za uhusiano……...……………………………. 13

1.8.1.2 Kanuni ya uhusiano katika mawasiliano…………………………. 14

1.8.2 Nadharia ya Uhusiano na ufasiri wa sitiari………………………. 15

1.8.3 Eksiplekecha…………………………………………………..... 16

1.8.4 Implekecha………………………………………………………17

1.8.5 Pragmatiki Leksika…………………………………………..…. 17

1.8.6 Pragmatiki Leksika na Nadharia ya Uhusiano……………………. 18

1.8.6.1 Ubanaji…………………………………………………..…… 19

1.8.6.2 Upanuaji ……………………………………………….. … 19

1.8.7 Dhana maalum ya kihali na nadharia ya uhusiano…………..…… 19

1.9 Mbinu za utafiti………………………………………………………. 21

1.9.1 Ukusanyaji wa data kutoka vitabuni……………………………… 21

1.9.2 Sampuli ya data…………………………………………………… 21

1.9.3 Uchanganuzi wa data…………………………………………………22

**SURA YA PILI: UAINISHAJI WA METHALI NA SITIARI …………….. 23**

2.1 Utangulizi………………………………………………………………… 23

2.2 Uainishaji wa methali za sitiari………………………………………........ 23

2.2.1 Methali za kisinedoki…………………………………………………23

2.2.2. Methali za kimetonimia…………………………………………..… 24

2.2.3 Methali za chuku……………………………………………….… 24

2.2.4 Methali za paradoksia……………………………………………….. 24

2.2.5 Methali za kitashibihi…………………………..………………… 24

2.2.6 Methali za Kisitiari….…………………………………….. …..…. 25

2.3 Historia na maendeleo ya Ufasiri wa sitiari ……………………………. 26

2.4 Uainishaji wa sitiari ……………………………………………………... 28

2.4.1 Uainishaji wa sitiari kulingana na Sperber na Wilson…………… 28

2.4.1.1 Sitiari huru ……………………………………………………….. 28

2.4.1.2 Sitiari funge………………………………………………. ………28

2.4.2 Uainishaji kulingana na Johnson na Lakoff…..………………… 29

2.4.2.1 Sitiari za kiishara (Konduiti)…………………………………… 29

2.4.2.2 Sitiari za kioriento……………………………………… …..... 30

2.4.2.3 Sitiari za kiontolojia…………………………………... …… 30

2.4.3 Uainishaji wa sitiari kulingana na Shelestiuk…………………..… 30

2.4.3.1 Uainishaji kiuamilifu………………………………………….. 30

2.4.3.2 Uainishaji wa kimuundo……………………………… …….. 32

2.4.3.3 Uainishaji wa kisemantiki …………………………………….. 33

2.5 Dhana ya sitiari dhanifu…………………………………………………… 34

2.6 Sifa za kijumla za sitiari dhanifu………………………………….……....35

2.7 Fenomena zinazohusiana na sitiari …………………………………..…. 36

2.7.1 Uhishi wa kisitiari au prosopopeia. ……………………………..… 37

2.7.2 Ufumbaji wa maongezi………………………………………………37

2.7.3 Antonomasia ya sitiari. …………………………………….. …….. 37

2.7.4 Sinesthesia. ………………………………………………..…….. 37

2.7.5 Ishara za kisitiari………………………………………………….… 38

Hitimisho………………………………………………………………………… 39

**SURA YA TATU: MAWASILIANO KUPITIA SITIARI DHANIFU………40**

3.1 Utangulizi……………………………………………………………..……… 40

3.2 Dhana ya maana ……………..……………………………………………… 40

3.3 Dhana ya muktadha……………………………………………………….. 42

3.4 Mikitadha katika utunzi wa methali za sitiari na chimbuko la methali… 42

3.4.1 Muktadha wa hali…………………………………………………… 42

3.4.2 Muktadha wa kijiografia…………………………………………… 43

3.4.3 Muktadha wa kitamaduni……………………………………………..44

3.4.4 Muktadha wa kihistoria………………………………………………44

3.5 Mawasiliano kupitia kwa sitiari dhanifu…………………………………… 48

3.5.1 Mawasiliano kupitia kwa sitiari za neno moja……………………48

3.5.1.1. Sitiari zinazorejelea vitu vya kudhania………………… …….. 49

3.5.1.2 Methali zinazotaja vifaa halisi……………………………………. 53

3.5.2. Sitiari zenye muundo wa kirai….……………………………………58

Hitimisho……………………………………………………………….…… .63

**SURA YA NNE: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO……… 64**

4.1 Utangulizi……………………………………………………………… 64

4.2 Muhtasari wa matokeo ya utafiti…………………………………………… 64

4.3 Hitimisho……………………………………………………………………… 65

4.4 Mapendekezo ……………………………………………………………….. 65

**MAREJELEO……………………………………………………………………66**

**VIAMBATISHO.**

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

Katika sura hii tutatoa muhtasari wa jumla wa tatizo la utafiti. Mambo yatakayoshughulikiwa ni pamoja na; historia ya utafiti, usuli wa mada, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, haipothesia, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, msingi ya kinadharia na mbinu za utafiti.

### 1.1 Usuli wa mada

Methali ni kipengele za fasihi ambacho huchunguzwa katika taaluma ya *Paremiolojia*. Methali zinahusishwa na mtaalam Archor Taylor ambaye anadaiwa kuwa mwanzilishi wa taaluma hii na wataalamu wa fasihi. Methali inaweza kufafanuliwa *kama msemo unaojitosheleza, wenye maana yenye nguvu au uzito, wenye muundo au sifa za kishairi, unaokusudiwa kuadibu au kuelekeza, kushauri na kadhalika* (Wamitila, 2001). Katika jamii ya kiafrika ambapo lugha ya masimulizi ina nafasi kubwa kwa watu wengi, methali bado zina nafasi na jukumu kubwa. Kulingana na madai ya wataalamu hawa ni kweli kusema kuwa methali ni usemi kamili ulio na maana na jukumu katika matumizi yake.

Methali zimejaa kwa kila mazungumzo, zinaweza kutumika kanisani, katika siasa, mahakamani na kwingine. Katika jamii nyingine za kiafrika, watu huweza kuteua mahali pa kuitumia methali kwa sababu, methali hubeba busara, hekima na zinahusishwa na uzoefu fulani, umri na cheo. Wale wanaotumia methali wanafaa kuwa wanaelewa lugha iliyotumika katika methali hizo (Bukenya et al. 1997). Methali hutolewa kama kauli zinazorejelea hali fulani za maisha. Zinaashiria mtazamo ya jamii kuhusu mazingira wanamoishi kwani “huchota” picha zake katika mazingira ya kimaumbile, vitu na fikira zinazoizunguka jamii, utamaduni na maisha ya watu fulani.

Methali huwa na sifa mbalimbali. Tulipozichunguza kwa kina tuliona kuwa methali huwa na sifa za kibalagha au chuku. Sifa ambayo hupatikana wakati tunachunguza maana ya methali kijuujuu wala sio kitamathali (Wamitila, 2001). Aidha sifa ya ukweli kinzani hupatikana katika methali. Ukweli kinzani husababishwa wakati kinachosemwa kama methali kinashughulikiwa kijuujuu.

Hivyo, sifa hii huzua utata ambao hutatuliwa kwa kuangalia maana ya ndani ya methali. Sifa ya tatu inayoonekana katika methali ni: maana batini na maana juujuu. Maana ya kijuujuu ni maana ya kisemantiki ilhali maana batini ni maana kimatumizi. Sifa ya nne ya methali ni ufunge (fixedness); ambapo msemo huwa haubadiliki. Mwisho, methali huwa na sitiari, sitiari ni mojawapo wa tamathali za kiusemi na maongezi inayotawala hata maongezi ya kila siku. Sitiari huweza kujenga sifa mbalimbali kama vile: za maono, masikizi, maonjo na mashiko.

Kingei (2008) na Robinson (2003) wanadai kuwa methali hujaa sitiari na hutumika katika mazungumzo kwa nia ya kuelimisha, kuasa, na kukejeli kwa njia iliyofumbwa na kuwekewa tasfida. Sifa hii ndiyo tulijikita kwayo katika utafiti wetu.

Kiini cha uelewa wa maana katika methali hutegemea uwezo wa kufasiri sitiari na mpangilio wa maneno yaliyotumika. Aidha, tamko hupewa maana kulingana na muktadha lililotokea katika mazingira ya kiutambuzi ya msikilizaji. Sitiari zilizotumika katika methali zina upana wa maana kwani, ufasiri wake hutegemea falsafa ya jamii, miktadha na uwezo wa kuchakata na kusaka maana. Inapotumiwa katika mazungumzo, maongezi au kwenye maandishi, sitiari hukuza picha fulani katika akili ya msikilizaji hivyo hufanya mawasiliano kuvutia na kunata akilini. Aidha, methali zina uwezo wa kukuza ujuzi wa jamii wa kuagiza na kujuza. Hivyo, sitiari zinafaa kuchunguza kwa kina, kwani uelewa wa methali katika mawasiliano huhusisha uwezo wa kuelewa maana na sifa ya sitiari.

Sitiari zimeainishwa na baadhi yaa wataalamu kwa msingi mbalimbali. Shelestiuk (2006) aliainisha sitiari kwa msingi ya kisemantiki (maana), kimofolojia (muundo) na kipragmatiki (kiuamilifu). Ricor (1997) naye akainisha sitiari kwa kuangalia muundo wa methali ambapo maana inaweza kupatikana katika leksimu inayorejelea dhana ambapo, dhana moja inalinganishwa na dhana nyingine kwa njia ya moja kwa moja. Sitiari za aina hii ndizo zinaitwa sitiari dhanifu na baadhi ya wataalamu kama vile Lakoff na Johnson (1986).

Maana halisi ya neno lililotumika katika sitiari dhanifu inaweza ikabadilika kabisa na neno likapata maana mpya. Kwa hivyo, huelewa wa methali za sitiari huhitaji mafikira ya kipragmatiki. Sitiari hizi zinapotumiwa, ujumbe unaodhamiriwa ama unaweza kupatikana au pengine ukakosa kueleweka au kufasiriwa ifaavyo. Hivyo, huelewa wa kimuktadha ambamo neno limetokea ni muhimu katika kuchunguza neno husika. Katika matumizi ya methali, kuna

ishara ambayo huwa na jukumu kuu katika methali nzima. Ishara inayopatikana katika methali ni zao la tajriba za jamii au mtu. Hivyo, maana hupatikana kwa msingi iyo hiyo kutoka akilini mwa msikilizaji.

Maana ya mtumiaji sitiari dhanifu hupatikana baada ya ujumbe kuchakatwa ubongoni mwa msikilizaji. Kupitia mchakato huu; usanii, maana na jukumu la neno hupatikana. Kinlon, (2005), alisema kuwa neno likitumika kisanii hupitisha ujumbe kisanii. Katika methali kuna misamiati mingi iliyotumika kisitiari: Kuna misamiati inayohusu wanyama wa porini, wanyama wa nyumbani, baharini au viumbe wa mbinguni, Aidha, kuna misamiati inayorejelea miti, sehemu za miti, mazao ya miti, aina za vyakula, watu, nyakati mbalimbali, wadudu na dhana dhahania. Misamiati hii hutumika kisanii kupitisha ujumbe.

Kwa kurejelea muundo, sehemu za methali, yaani sehemu ya swali na ya jibu huweza kuwa leksimu inayolinganishwa na leksimu nyingine kwa njia ya moja kwa moja.
Tazama:

*Ubishi ni ghasia*
*Toba ni kitendo*
*Cheo ni dhamana.*

Leksimu zifuatazo zimetumika kama sitiari: ghasia, kitendo, dhamana. Sifa moja ya kimuundo ya sitiari ni kuonyesha uhusiano baina ya vitu, hali, au hata sehemu mbili au zaidi kwa kuzilinganisha moja kwa moja. Inavyoonekana ni kuwa sifa za *ghasia*, *kitendo* na *dhamana* zinabandikwa *ubishi*, *toba* na *cheo* ili kurejelea hali halisi kuhusu ulimwengu. Uelewa wa ishara hizi utategemea muktadha ambamo neno kistiari limetokea na utahusu upanuzi wa neno hili kwa msingi ya dhana maalum ya kihali.

Methali zimeshughulikiwa sana na baadhi ya watafiti kwa msingi ya kifasihi. Machache yametafitiwa kiisimu kuhusu methali. Methali huwa na sitiari za kila aina. Baadhi ya sitiari katika methali ni sitiari dhanifu. Utafiti huu unalenga kuchunguza maana ya sitiari dhanifu katika methali kwa misingi ya isimu. Tulichunguza namna neno hubadilisha maana yake halisi katika muktadha wa kulinganishwa na neno lingine na kuonyesha namna mabadiliko hayo yanayoafikiwa kwa misingi ya nadharia ya uhusiano.

## 1.2 Tatizo la utafiti

Dhana ya sitiari ni muhimu kutazamwa kwa sababu ama ni njia moja ya kuwasilisha ujumbe kwa njia inayovutia na kutia ladha kwenye lugha au kuficha ujumbe mzito au zote mbili. Imedhihirika kuwa neno linalotumika kisitiari linabadilisha maana yake halisi na kupata maana mpya. Mabadiliko hayo hutokea katika harakati za kutafuta maana ya msamiati uliotumika katika sitiari.  Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu sitiari ila hakuna utafiti umefanywa kuhusu methali za sitiari dhanifu za lugha ya Kiswahili. Utafiti huu unalenga kuchunguza namna dhana hupata maana mpya kupitia kwa dhana nyingine.  Ni bayana kwamba dhana chanzi (dhana ya pili) inayopatikana katika sitiari dhanifu hubadilisha maana yake halisi katika matumizi ya sitiari na kupata maana mpya. Tutachunguza namna maana mpya huzalika baina ya dhana au leksimu inayolinganishwa katika methali za sitiari za Kiswahili. Utafiti ulichunguza sifa za dhana au maneno yaliyotumika kama sitiari katika methali za aina hii kwa msingi ya nadharia ya uhusiano**.** Nadharia hii ni muhimu katika kubainisha namna uhusiano baina ya dhana huzalisha maana mpya katika akili tambuzi ya msikilizaji.

## 1.3 Madhumuni ya utafiti

a. Kubainisha  mikabala mbalimbali inayoweza kutumika kuainishia methali za sitiari ya Kiswahili.
b. Kuchanganua uhusiano wa sifa za ishara na namna uhusiano huo huzua fahiwa ya maana.
c. Kuchunguza athari za kimuktadha katika diskosi za methali.

## 1.4 Nadharia tete

a. Kuna mikabala mbalimbali ya kuainishia sitiari iliyopo katika methali za sitiari dhanifu ya Kiswahili.
b. Fahiwa za maana katika methali za sitiari dhanifu, huwezeshwa na uhusiano wa sifa za ishara zinazolinganishwa.
c. Katika matumizi, majukumu ya methali za sitiari hutofautiana katika muktadha halisi na muktadha wa kisaikolojia

### 1.5 Sababu ya kuchagua mada

Kufasiriwa kwa lugha kitamathali, haswa sitiari dhanifu, wakati mwingine kunaweza kuwa na ugumu unaotatiza mawasiliano. Hii ndio sababu tumechagua sitiari dhanifu katika methali kama sehemu ya uchunguzi wetu. Utafiti huu unachukulia kuwa lugha ni hazina kubwa ya binadamu katika mawasiliano. Lugha yoyote ulimwenguni inaweza kutumika kiishara, kama vile, kwa misingi ya kitamaduni, dhana fulani unahusishwa na dhana nyingine, mfano: *Ua la waridi* kuhusishwa na *umaridadi au mapenzi.* Sitiari dhanifu hulinganisha wazo au dhana moja na nyingine, hivyo ni lazima uhusiano baina ya dhana uchunguzwe na uafikiwe ndivyo maana ipatikane. Aidha, sitiari hii inahitaji kushughulikiwa kwa kina na watumiaji katika akili zao ili ujumbe upitishwe, na falsafa zinazobebwa na jamii zipatikane, kisha maana yake ieleweke.

Methali zenye sitiari ya leksimu moja au kirai zinapotumiwa katika mazungumzo, maandishi, na kwenye matangazo, msemaji hutarajia kuwa anayesikiliza au anayesoma ataelewa maana ya tamko au maandishi hayo. Lo Liyong, (1985), alisisitiza zaidi kuwa tutambue majukumu yanayoweza kutekelezwa na amali za kiasili kwa manufaa ya jamii ya leo. Hivyo, fafanuzi za sitiari dhanifu hazijashughulikiwa kwa msingi ya kumsaidia msomaji au msikilizaji kuelewa maana kikamilifu. Wasomi wanatatizika kuipata maana iliyokusudiwa. Sababu mbalimbali zinaweza kuelezwa kama zinazochangia kutoeleweka kwa maana ya sitiari dhanifu, nazo ni kama vile: kutokuwa na fafanuzi za dhana za leksimu tumika, pili kubadilika kwa maana ya neno kisemantiki kulingana na muktadha.

Kitanzu hiki kinapotumiwa katika mawasiliano baina ya watu wawili; msemaji na msikilizaji. Msemaji hutarajia msikilizaji amwelewe ndipo mawasiliano yakamilike, hivyo, msikilizaji anafaa kulichakata neno hadi aipate maana, kisha, atoe jibu linalohusiana na tamko la msemaji. Ikiwa msikilizaji hatapata maana ya msemaji, basi mawasiliano hayatafaulu. Utafiti huu utachangia katika utafutaji wa maana iliyoko kwenye sitiari. Kwa msingi ya kanuni za nadharia ya uhusiano, hivyo inakusudiwa kuwa utapunguza utata unaozuka baina ya wazungumzaji hasa, katika kufasiriwa kwa sitiari dhanifu katika methali.

Watafiti mbalimbali wameangalia tamathali mbalimbali za lugha, kama vile: nyimbo na vitendawili. Hakuna lililofanywa kuhusu sitiari dhanifu kwa msingi ya isimu. Mtafiti ananuia

kuziba pengo kwa kutoa mchango wa kiusomi kuhusu kijitanzu hiki muhimu za fasihi kwa kuchunguza namna maana za sitiari dhanifu hufikiwa kupitia mahusiano ya dhana linganishwa katika methali. Pia tunatarajia kutoa mchango kwa tafiti zilizofanywa pamoja na zile zitakazofanywa baadaye katika nyanja hii vilevile wanaotaka kuandika mengi kuhusu sitiari za Kiswahili na wale wanaotaka kuandika ensaikilopedia za sitiari watafaidika pakubwa.

## 1.6 Upeo na mipaka ya utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza sitiari dhanifu zilizo katika methali za Kiswahili, kwa kuonyesha namna maana halisi ya leksimu, iliyotumika kisitiari, hubadilisha maana na kupata maana nyingine tofauti katika mutadha wa matumizi. Tulichunguza uhusiano wa dhana inayoashiriwa na leksimu na namna mahusiano ya dhana linganishwa huzua maana ya methali. Mtafiti alimakinikia sitiari dhanifu kwa kulenga leksimu ya dhana chanzi (DC) na namna inavyohusiana na dhana lengwa (DL) katika kuleta kuleta mabadiliko ya maana.

Mtafiti alijikita katika uainishaji wa sitiari uliopendekezwa na Ricour (1997), ili kubainsha muundo wa sitairi dhanifu, na Shelestiuk (2006) ambaye aliainisha sitiari kwa kufuata kigezo mbalimbali vikiwemo vigezo vya muundo. Ricour alipata aina mbili za sitiari zinazopatikana katika methali: alisema kuwa kuna sitiari huru ambazo maana yake ueleweka kutoka kwa leksimu, kuna zingine ambazo ufasiriwa katika viwango vya kirai, kishazi, na hata sentensi nzima: sitiari funge.

Mtafiti alilenga kushughulikia methali za sitiari kwa kuchunguza mahusiano baina ya dhana husika, na namna yanavyoathiri fasiri za neno, kwa msingi ya enisaikilopedia na kijamii. Alitumia nadharia ya uhusiano ya Sperber na Wilson. Nadharia ambayo ilitupatia nuru ya kuelewa na kufasiri ujumbe uliosimbwa, maana kisemantiki, na ile uliojengeka katika miktadha ya kiurejelezi kwa msingi ya utaratibu fahamishi na dhana ya *ad-hoc*, ambazo hujishughulisha na uhusiano uliopo kati ya maana na muktadha; ikiwemo muktadha ya ndani na ya nje.

## 1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada

### 1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu methali

Salwa (2005) alifanya uchunguzi kuhusu fafanuzi za methali, aliwauliza watu waandike fasili za neno methali, aliweza kuafikia kuwa kuna ukubaliano fulani kuhusu methali. Ilibainika kuwa methali huwepo katika kila lugha, na watu wamekuwa wakizitumia kueleza uelewa wao kuhusu imani, desturi na mazingira yao ya kawaida. Aidha, zinapitishwa kwa njia ya mdomo kupitisha utamaduni wa binadamu. Utafiti wake Salwa ulitusaidia kupata fafanuzi za methali.

Bukenya et al (2005), Meider (2005) walisema kuwa "methali huwa na umuhimu sana katika mazungumzo ya binadamu katika hali yoyote ile, iwe ya kimaandishi au ya mazungumzo." Methali zinaweza kutumika kutekeleza majukumu mbalimbali kama vile kueleza uhusiano wa kimamlaka, jinsia au hata umri (Njagi 2013). Zaidi ya hayo, Njagi alichunguza namna methali hueleza mamlaka ya kisiasa katika lugha ya kiembu. Madai kuwa methali zinaeleza aina mbalimbali za uhusiano ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu tulinuia kuchunguza sitiari kama zinavyotumika katika mazungumzo au maandishi.

Soi (2014) alifanya uchunguzi kuhusu jukumu la sitiari za Kipsigis katika tarafa ya Kaptundo. Alifaulu kupata majibu yafuatayo kutoka kwa washiriki. Kwanza, kulingana na baadhi ya washiriki, methali ikitumika katika muktadha ufaao, inaweza kutumika kuonya, kuelimisha kushauri, au kukuza lugha kwa mtu binafsi au jamii. Baadhi ya malengo yanaweza kuwa: kushutumu tabia zisizofaa katika jamii, kuficha ujumbe ili usipitishwe kwa mtu asiyekusudiwa, kulinganisha matukio na kuonyesha uwezo wa kiakademia wa mwanadamu

### 1.7.2 Yaliyoandikwa kuhusu sitiari

Tafiti nyingi zimeandikwa kuhusu sitiari, baadhi ya wataalamu walishughulikia sitiari ama kimatumizi, kimuundo au kisemantiki. Hivyo, fasiri ya sitiari ni tata. Imekuwa tatizo kwa muda mrefu kusawazisha fasiri ya sitiari. Tafiti kuhusu sitiari kwa msingi mbalimbali zimefanywa na wataalamu mbalimbali wameibuka ni njia zao za kufafanua sitiari. Baadhi ya watafiti wameangalia na kuchunguza sitiari kama upanukaji wa maana halisi kwa msingi wa neno, kama vile: (Carston na Wilson 2007), Onish na Murphy (1993). Walisema kuwa maana kisitiari haiwezi kueleweka kwa urahisi ikilinganishwa na maana halisi ya neno. Onish na Murphy (1993) walisema kuwa "ufasiri wa yale anayotaka kusema msemaji hayawezi kutoa maana kwa

kuangalia neno pekee. Lazima neno lihusishwe na muktadha wa usemi." Yule (2010) alitetea suala la kuhusisha muktadha katika kupata maana. Alieleza namna tunavyoweza kutumia maana za neno, muktadha ambao neno hutokea, ujumbe wa awali kama njia ya kutafuta maana ya msemaji anayetoa ishara fulani kwa nia ya kuwasiliana. Ufasiri wa maana ya ishara haujikiti katika neno pekee bali kwa kile tunachofikiria kuwa msemaji alinuia kukisema. Mawazo haya ni muhimu sana katika kufasiri maana ya sitiari inayopatikana katika methali, kama njia ya kupata maana ya msemaji au ya matini.

Pili, baadhi ya wataalamu waliona sitiari kama uhamishaji wa maana (Myers na Simms 1978), Wales (1978), Nurberg (2004). Nurberg alisema kuwa uhamishaji huu hutokana na kuhamishwa kwa sifa za kisemantiki za kitu kimoja hadi kingine ambacho kina sifa sawa na kile kinachojulikana. Myers na Simms (1978) na Wales (1978) wote walisema kuwa sitiari inahusu huhamishaji wa maana ambapo muktadha wa matumizi ni muhimu katika kurejelea maana.

Tatu, baadhi ya wataalamu wanaona sitiari kama ufafanuzi wa kitu kimoja kwa msingi ya kitu kingine. Wao ni kama vile: Leech (1965), Cuddon (1979), Cruse (1986). Cruse (1986) Alitetea kuwa sitiari humshawishi msikilizaji au msomaji kutazama vitu, hali au tabia ya kitu kimoja kama kitu kingine kwa kutumia maelezo ya kiisimu yanayorejelea dhana moja sawa na nyingine. Alisisitiza kuwa sitiari ni kiungo muhimu cha kiutambuzi ambacho ni dhanifu na tajriba ya vitu dhahania na visivyohisika vinaweza kudhahaniwa kuwa vinafahamika na viko imara.

Cuddon (1979: 391) alisisitiza kuwa ulinganifu wa sitiari ni wa kiumaanisho. Alitofautisha ulinganifu wa kitashbihi na ule wa kisitiari kwa kudai ulinganifu wa kitashibihi huwa wa maana wazi. Leech (1965), alishikilia msimamo karibu na ule wa Cuddon, anadai kwamba katika sitiari, vitu viwili au zaidi ambavyo havifikiriki kuwa na mshikamano au muungano na vitu vingine huletwa pamoja na kuunganika katika udhanifu wa kile kingine. Hivyo, kipragmatiki, sitiari ni aina moja ya upanuaji ambapo maana iliyowasilishwa huwa tofauti na maana leksika ya neno. Wataalamu hawa wanapatana kuwa maana ya neno lililotumika kisitiari lazima ipanuliwe kwa msingi ya ulinganishi wa sifa. Onish na Murmpy (1993:115) waligundua kuwa maelezo ya kisitiari si rahisi kueleweka kama maelezo halisi. Hii ni kwa sababu maana kisitiari inaweza kuwa na fasiri mbalimbali na inahitaji data za kiensaiklopedia ili kutatua utata. Data tunayoichunguza, inahitaji data za kiensaiklopedia pamoja na uundaji wa dhana maalum ya

kihali ili kufasiriwa. Assimakopoulos (2008) aligundua kuwa, katika kufasiriwa kwa tamko, maana iliyosimbwa inaweza kubadilika kipragmatiki na kumlazimisha mtu kuunda dhana maalum ya kihali katika hali hiyo. Utafiti wake ni muhimu kwa sababu ufasiri wa sitiari dhanifu unahitaji uundaji wa dhana maalum ya kihali.

Sitiari, pia ilichunguzwa kimatumizi na baadhi ya wataalamu kama vile Ndirangu (2011) Todoli (2007) na Faycel (2008). Faycel (2008) alichunguza sitiari zinazotaja maneno ya aina za chakula katika methali za Kiarabu nchini Tunisia kwa kutumia Nadharia ya Sitiari ya Lakoff (1993) na Nadharia Kuu ya Kudhibiti Sitiari ya Lakoff na Turner (1989). Ndirangu (2011), Alichunguza matumizi ya sitiari katika idhaa za redio za kiasili nchini Kenya. Alieleza jinsi lugha ilivyotumiwa katika mwaka wa 2007 kabla na baada ya ghasia za uchaguzi mkuu wa mwaka huo. Utafiti wake utasaidia kujua namna sitiari zinafaa katika kuficha maana kimatumizi. Matumizi haya ya sitiari pia yaliungwa mkono na Kobia (2008) Alipodai kuwa sitiari hutumiwa kuficha aibu na kuyafanya mambo mazito kuwa mepesi. Haswa, ikiwa maneno hayo ni mwiko kutamkwa hadharani. Kwa kutumia dhana au picha ambazo zinafahamika na kueleweka na umma ambapo baadhi ya sitiari hupatikana katika semi, (Todoli 2007). Utafiti wake ni nuru katika utafiti wetu, kwani, utafiti wetu ulishughulika na semi za aina hii.

### 1.7.3 Yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya uhusiano

Nadharia ya pragmatiki leksika na ile ya uhusiano haiwezi kutenganishwa, baadhi ya wataalamu wanaotumia nadharia ya uhusiano hujikuta wamejikita katika baadhi ya msingi ya nadharia ya pragmatiki leksika. Nadharia ya uhusiano inaongozwa na utafutaji wa uhusiano, inajihusisha na umaanisho na hujikita katika pragmatiki leksika, (Sperber na Wilson 2004).

Grice (1963) alidai kuwa mawasiliano yanaweza kuafikiwa kwa urahisi ikiwa msemaji atawafanya/atamfanya wasikilizaji/msikilizaji aitambue nia yake na watambue kuwa tamko lake linaafikia kiwango fulani kilicho na maana kwa msemaji. Katika kazi yake, Grice alitarajia kuonyesha namna fikira za maana ya msemaji, zikichunguzwa kwa msingi ya nia, zingetumiwa kiisimu kujenga wazo imara la maana ya sentensi au neno. Alieleza kuwa mawasiliano kwa njia iliyo wazi yanaweza kutokea kiubunifu. Hivyo, alipendekeza seti za kanuni za mahusiano

zilizoundika katika kanuni ya ukweli, idadi, mahusiano na namna. Kanuni hizi ni muhimu katika nadharia ya uhusiano ambayo ndio nadharia kuu katika utafiti huu.

Wilson na Sperber (2004) waliuona udhaifu wa nadharia ya ushirikiano ya Grice wa kutoweza kueleza kikamilifu namna ushirikiano wa wahusika huchangia kufaulisha mawasiliano pamoja na kueleza maana inayokusudiwa na msemaji, ndipo wakaunda nadharia ya uhusiano. Kupitia nadharia ya uhusiano, walidai kuwa usemi huweza kuwa na uhusiano ikiwa kile anachosema mtu kitapata uhusiano katika akili ya msikilizaji. Kulingana nao, mawasiliano huongozwa na kanuni ya uhusiano ambayo ndiyo huchuja habari kwa kuchunguza kiwango cha uhusiano. Hivyo, kuna habari zenye uhusiano wa kiwango cha juu zingine kuwa na kiwango cha chini. Habari zenye uhusiano wa juu hutumia gharama ya chini kufasirika na zilizo na uhusiano wa chini zina gharama ya juu kufasirika. Kazi ya Sperber na Wilson ni nguzo katika kutathimini kiwango cha kufasiri sitiari.

Watafiti waliotumia nadharia ya uhusiano kutafiti mambo mbalimbali ni kama vile Blutner (1999) aliyebainisha kuwa pragmatiki leksika inachunguza msingi ambayo maana kiisimu ya neno, inaweza kubadilika katika matumizi. Katika hali hii, sitiari katika methali zilifasiriwa kwa msingi ya muktadha ya kimatumizi. Muktadha ni muhimu sana kupata maana ya sitiari, (Liu 2006, Schroeder 2005), Habwe (1999). Pragmatiki Leksika inaongozwa na utafutaji wa uhusiano (Sperber na Wilson 2004). Maoni haya yataongoza ufasiri wa sitiari katika diskosi ya methali kwani swala la muktadha lina umuhimu mkuu katika kutafuta maana ya semi.

Tarjan na Nurkamtoin (2013) walifanya utafiti kuhusu kile walichokiita matamshi ya kiushwawishi yaliyotumiwa na wanakampeni wa Regent na Vice Regent katika uchaguzi wa Pasuruan; Mashariki ya Java. Uchunguzi wao ulilenga kuangalia kiolezo, mikakati, na kanuni za kijamii na kitamaduni za kauli zinazoshawishi, ambazo hutumika katika kampeni za kisiasa kwa mtazamo wa kipragmatiki leksika. Pencis na Uzule at al. (2011) walifanya tafiti wa kipragmatiki wa jumbe za kisiasa katika mtandao wa twita wa Latvian wakati wa uchaguzi mkuu 2010, wakafanya uchanganuzi wa majadiliano ya kisiasa, hashitagi na utwitaji-upya (*retweeting)* wa jumbe. Walilenga kubainisha wazi tofauti kuu kwa msingi ya masafa ya kiuhalisi *(physical distance)* na kiutambuzi baina ya watu binafsi na makundi, katika mchakato ya kuunda ubainishaji, hivyo, walipendekeza haipothesia ambayo ilibainisha wazi mahusiano baina ya watu binafsi na kundi la watu, utajirishaji wa mada, vifaa vya mawasiliano na frekwesi ya kutaja

udokezaji na athari za ujumbe kwa nia ya kuchunguza ni vipi muktadha huathiri uelewa wa jumbe. Utafiti wao ulitusaidia, kwa sababu utafutaji wa fasiri ya sitiari uhitaji muktadha na sifa mbalimbli za kiensaiklopedia ili kuipata maana ya sitiari katika kuwasilishwa ujumbe kwa kutumia sitiari.

Kinyua (2012), katika utafiti wake wa kusimbua vibonzo, alitumia mtazamo wa pragmatiki kuchanganua vinyago katika gazeti la *Daily Nation*, utafiti wake ulinuia kutalii nia ya kutumia vinyago kuwasilisha, kwa njia fiche, masuala hatari yanayoathiri jamii ili kuleta mabadiliko chanya ya kisiasa na kijamii nchi Kenya. Utafiti wake ulibainisha maana wazi na fiche katika kuwasiliana kupitia matumizi ya vinyago. Ilihitimishwa kuwa matumizi ya vinyago huhitaji utajirishaji huru wa umbo la kisemantiki linalonuia kuwasilisha dhana iliyosimbwa na ambayo huwa na maana zaidi ya kiisimu. Suala la utajirishaji ni muhimu katika kufasiri sitiari kwani maana kisitari huhitaji kutajirishwa ili ifae muktadha wa matumizi.

Methali huangaliwa kama diskosi kwa sababu inahusika katika mazungumzo na hubeba mambo mengi kuhusu usemi, kama vile: falsafa, maana, utamaduni na nia, (ikiwa itawasilishwa kwa mdomo) au kama tini (ikiwa itawasilishwa kwa maandishi). Wataalamu kama vile Schiffin, (1994) alichunguza mtazamo sita tofauti ya kuchunguza diskosi. Naye Johnstone (2001) akachukulia uchanganuzi wa diskosi kama uwanja wenye mtazamo kadha isiyo funge. Alionyesha mbinu tofauti za kuchanganua diskosi, baadhi ya mitazamo hii ni kama vile: mtazamo rasmi, mtazamo wa kukokotoa, wa kiisimujamii na kipragmatiki. Mtazamo wa kipragmatiki ndio uliopendelewa na ndio tutatumia katika tafiti huu.

## 1.8 Msingi wa kinadharia

Nadharia ya uhusiano iliasisiwa na Wilson na Sperber (1986) na kuendelezwa mwaka wa 2004. Nadharia hii inatokana na udhaifu wa nadharia ya ushirikiano ya Grice kwa kutoweza kueleza kikamilifu namna ushirikiano wa wahusika huchangia kufaulisha mawasiliano, pamoja na kueleza maana inayokusudiwa na msemaji. Nadharia ya uhusiano hujihusisha na umaanisho, hivyo, husaidia katika kuafikia uandishi wa enisaikilopedia. Inajikita katika pragmatiki leksika na hujaribu kuunganisha kanuni za Grice na kanuni za mawasiliano na kuunda kanuni moja ya uhusiano.

Nadharia hii ilitupatia nuru ya kuelewa na kufasiri ujumbe uliosimbwa, maana kisemantiki na ile iliojengeka katika miktadha ya kiurejelezi. Nadharia hii pia hushughulika na uhusiano uliopo kati ya maana na muktadha; ikiwemo muktadha ya ndani na ya nje. Husaidia kuelewa lugha hasa pale tamko huweza kuwa na maana tata; hasa lugha kitamathali au kishairi. Kueleweka kwa maana huchochewa na mikakati ya urejelezi katika akili ya msikilizaji.

### 1.8.0 Madai ya nadharia ya uhusiano

Kulingana na Wilson na Sperber, nadharia ya uhusiano (NU) ina madai yafuatayo. Kwanza, utafutaji wa uhusiano ni sifa kuu ya akili ya binadamu. Kulingana na NU mwanadamu ana tabia ya kutumia uhusiano kwa kiwango cha juu kwa sababu akili yake huwa hivyo. Katika hali ya kurahisisha utendakazi, mitazamo ya kiutendaji hulenga kukichukua kichochezi (*stimuli)* kilicho na uhusiano zaidi, nao utendaji-rejelewa wetu wa kiakili ukawezesha chukulizi zilizo na uhusiano mkuu, nao utendaji rejelezi hulenga kukichakata kichochezi hiki kwa njia yenye maufaa zaidi (kanuni tambuzi za nadharia ya uhusiano).

Pili, pembejeo kama vile tamko, mwangaza, kumbukumbu au sauti huwa na uhusiano kwa binadamu wakati inapata mizizi katika jumbe za awali alizo nazo msikilizaji au msomaji. Ujuzi wa awali wa msikilizaji, humsaidia kupata hitimisho lililo na maana kwake. Pembejeo huwa na uhusiano kwa mtu wakati inachakatwa katika misingi ya chukulizi zilizopo ili kuleta athari tambuzi chanya. Kulingana na NU, pembejeo ina uhusiano kwa mtu wakati itachakatwa na athari tambuzi chanya kupatikana. Athari tambuzi hufikiwa kwa kuchakata pembejeo katika muktadha wa umaanisho kwa kuhusisha pembejeo hiyo na muktadha.

Tatu, wakati wa tamko, inafaa tamko liunganike na muktadha hili uhusiano huafikiwe, Mkutadha, unafafanuliwa kama ujuzi alionao msemaji na anaoutumia katika mawasiliano. Unaweza kufafanuliwa kama seti za chukulizi zinazotumiwa kufasiri tamko (Sperber na Wilson 1995). Muktadha ni sehemu muhimu ya kisaikolojia ya msikilizaji inayochangia kuundia seti ndogo za chukulizi kuhusu ulimwengu au jumbe zilizo na maana ambazo zinahifadhiwa katika akili ya mtu wakati wa kutamka/ kutamkwa kwa neno.

### 1.8.1 Kanuni za kinadharia ya uhusiano

#### 1.8.1.1 Kanuni tambuzi za uhusiano.

Kulingana na Sperber na Wilson (1995: 260), utambuzi wa mwanadamu huonekana kuelekeza uangalifu na uwezo wa uchakataji kwa tamko lililotamkwa ili kuzidisha uhusiano wa pembejeo inayochakatwa. Kwa sababu ya msukumo wa kiuteuzi katika kuongeza ufaafu wa utambuzi; utaratibu wa kiutambuzi wa binadamu hulenga kuteua moja kwa moja pembejeo zenye uhusiano unaofaa zaidi, nao utaratibu wa kusaka kumbukumbu huelekea kuteua moja kwa moja chukulizi za kimauhusiano ya muktadha zinazofaa, nao mfumo wa kiurejelezi huchakata pembejeo hizi kwa hiari na kwa njia iliyo bora ya uzalishaji. Hivyo basi, mawasiliano yetu yanafaa kubashiri kwa kiwango fulani, kichocheo ambacho msikilizaji anaweza kushughulikia, uchukulizi wa kimuktadha anaoweza kuutumia katika kuichakata pembejeo na hitimisho ambayo anaweza kuipata kutokana na tamko.

Wilson &Sperber (2004) walisema kuwa usemi huwa na uhusiano ikiwa unaoana na habari za awali ambazo zimo ubongoni mwa msikilizaji kuhusu kile kinachosemwa- uhusiano huu ndio husaidia katika kufanya uamuzi wa kile kinachodhamiriwa na msemaji katika usemi wake. Kulingana na Sperber na Wilson (1995), utambuzi wa mwanadamu hulenga kutumia uhusiano kwa kiwango kikubwa. Wanadai kuwa ishara pokezi kama vile:- kuona, kutamka au kumbukizi ni muhimu kwa mwanadamu ikiwa zinaingiliana na fikira alizonazo msikilizaji, ambazo humsaidia kuhitimisha vyema kilicho na maana kwake. Mafikira ni uwezeshaji wa hali fulani hivyo huunganisha ishara mbalimbali kwa nia ya kuzalisha uchukulizi utakaosaidia katika kuhitimisha lengo la msemaji. Yaani mawasiliano hupitia mchakato ufuatao: Msikilizaji hutumia uwezo wao kusoma nia ya msemaji kwa kutumia urejelezi fulani alio nao kuanzia kwa kichochezi--- muktadha----uhusiano.

Kichochezi hiki kinaweza kuwa mafikira, maigizo, matamshi, ujumbe mfupi. Kichochezi huunganika na muktadha katika mazingira ya kiutambuzi ya msikilizaji na kupewa ufasiri katika mazingira yaleyale ya kiutambuzi. Athari za utambuzi ni uwezeshaji wa akili na uundaji upya wa akili. Athari hizi zinaweza kuimarisha ujumbe wa awali, kuudhoofisha ujumbe wa awali au kuleta uchukulizi mpya.

Sperber na Wilson (1995) walidai kuwa ujumbe mpya ni muhimu katika muktadha wowote ambao una umaanisho wa kimuktadha- wanasema kuwa kiwango cha umaanisho wa kimuktadha

hutegemeana, hivi kwamba, ikiwa umaanisho kimuktadha ni wa kiwango cha juu, vile vile uhusiano huwa vivyo hivyo. Ikiwa ujumbe mpya huafikia uhusiano kwa kuimarisha uchukulizi za awali, basi, huafikia uhusiano kwa kuondoa au kupinga uchukulizi awali. Gibbs (1994) akirejelewa Wilson (2006), alisema athari tambuzi huafikiwa wakati tamko la msemaji huimarisha uchukulizi wa awali, huongeza ujumbe mpya, au huupinga ujumbe wa awali, yaani mawasiliano hutokea katika msingi ya pata-potea. Hivyo, msemaji na msikilizaji huongozwa na hamu ya kusaka uhusiano wa kiwango cha juu, hivi ni sawa na kusema kuwa, ujumbe ambao una uhusiano mkubwa sana kwa msikilizaji humfaidi sana na hutumika katika mchakato na hurahisisha uhitimishaji. Ujumbe mpya unahusiana ikiwa una athari za kimuktadha hivi kwamba-athari za kimuktadha zinapokuwa nyingi, uhusiano wa ujumbe huwa mwingi pia. Ujumbe hupata maana kwa msikilizaji ikiwa utaunganika na muktadha. Katika ufasiri wa matamshi, kwa msingi ya kiurejelezi, kuna utumiaji wa kijesehemu kidogo cha mazingira tambuzi kilicho na uchukulizi maalum ambacho huletwa na kudumishwa na msikilizaji.

Kulingana na Sperber (1995) hitimisho hupatikana wakati tamko linachanganuliwa katika mikitadha ya akili kwa kulinganishwa na yaliyo kwenye akili. Uchanganuzi huu ndio huzaa ujumbe mpya ambao hukuzalika kutoka kwa matamshi au kutokana na jumbe za awali. Nadharia hii ni bora sana kwani inaweza kutumiwa katika kufasiri, kuchanganua na kuchakata sitiari.

### 1.8.1.2 Kanuni ya uhusiano katika mawasiliano

Kanuni hizi ndizo huongoza utaratibu wa kuchakata na kufasiri ujumbe, ndizo huchuja habari katika akili ya kiutambuzi ya msikilizaji kutegemea kiwango cha uhusiano - yaani kinachofahamika au kilichosemwa kinatoa uhusiano fulani ambao huchangia kupata fasiri ya maana aliyokusudia msemaji. Hivyo, nadharia ya uhusiano ina msingi yake katika pragmatiki leksika, kwa sababu inaundika katika mchakato wa kiutambuzi wa upokezi na huchunguzwa kwa msingi ya fikira za athari za kiutambuzi.

Nadharia ya uhusiano inadai kuwa mawasiliano huunda jumla ya uhusiano. Msikilizaji wa tamko hupewa haki ya kutarajia kuwa tamko litakuwa na uhusiano unaotosha na unaostahili kuchakatwa, zaidi, tamko lafaa kuwa na uhusiano na lioane na uwezo na matarajio ya msemaji. Jambo hili husababisha utaratibu fahamishi ambao, kulingana na nadharia ya uhusiano, bila shaka, hutumiwa na mtandao ya akili kushughulikia pembejeo husika. Msikilizaji huchukua maana kiisimu, kulingana na njia finyu ya nguvu za uchakataji; anaitajirisha katika kiwango cha eksiplekecha na kuikamilisha katika kiwango cha implekecha mpaka maana itakayopatikana hitimishe kiwango cha uhusiano.

Ufasiri wa tamko huna matokeo mawili kwa pragmatiki leksika; kuna maana iliyosimbwa ya neno kiisimu au kirai au sentensi; huwa na ishara ya kuonyesha bayana maana ya msemaji inayorejelewa na maana isiyo dhahiri. Kuelewa maana ya tamko lolote, iwe maana wazi au maana kisitiari ni jambo la kuona uhusiano unaotarajiwa, ili kuona uhusiano unaotarajiwa wa tamko kuna haja ya kufuata njia zenye ufinyu katika urekebishaji jozi wa maana wazi, muktadha na athari tambuzi kama inavyoelezwa bayana katika utaratibu fahamishi wa nadharia ya uhusiano.

Katika nadharia ya uhusiano, mawasiliano huonekana kama masuala ya kijamii kwa sababu yanahusishwa na mwingiliano ya kijamii. Uwezo unaohitajika katika mawasiliano hulenga zaidi dhana kuliko hisia za wanaongea. Kinachohitajika baina za wazungumzaji ni kutoa ishara; na anayefasiri anahitajika kushughulikia ishara hiyo.

Mawasiliano ya kiurejelezi ni muhimu katika jamii kwa sababu yanachunguza na kupanua mipaka ya maneno katika mazungumzo. Ujumbe huwa na uhusiano wa juu ikiwa akili ya msikilizaji itapata uhusiano wake kwa urahisi na kuufasiri kwa gharama ya chini (Blass 1990). Michakato ya kufasiri semi hutegemea kigezo cha uhusiano (Sperber 2004) na michakato hii inaweza kupuuza fasiri mbalimbali na kukubali fasiri moja ambayo huwa ndiyo yenye uhusiano wa hali ya juu – mchakato wenyewe hukoma pale msikilizaji anapopata au kukosa uhusiano wa kilichosemwa na msemaji.

### 1.8.2 Nadharia ya uhusiano na ufasiri wa sitiari

Mhimili mkuu wa kanuni ya mawasiliano katika uhusiano ni; mawasiliano huwa tendo la kutamka ambalo huwa na kiwango cha uhusiano kwa msikilizaji. Uchakataji sitiari huhitaji utafutaji wa uhusiano wa sifa za vitu viwili mpaka maana tarajiwa ufikiwe, kwani sitiari huwa na maana mbili:-*Maana wazi au maana ya moja kwa moja*. Pia huitwa eksiplekecha au maana kisemantiki, ambapo maana iliyosimbwa katika neno na hufasiriwa moja kwa moja. Maana hii hufasiriwa kwa urahisi. Maana ya pili ni *maana iliyofichama au ya ziada* ama implekecha au maana kipragmatiki. Hii ni maana ya msemaji ambayo msikilizaji anatarajiwa kuielewa. Maana hii ueleweka tu inapowekwa kwenye muktadha wa matumizi. Maana hii huhitaji mchakato wa akili ili kutafuta uhusiano na kupata ujumbe wa msemaji. Ufasiri wa maana hufanyika katika akili ya msikilizaji, na hupitia katika mchakato ufuatao kulingana na Akmajian (2001).

wazo

↓

Uwezo wa utambuzi wa usemi

↓

Uwezo wa kuelewa mfumo wa kileksika na kisintaksia

↓

Uwezo wa ufasiri wa kisemantiki

↓

Uwezo wa kufasiri kipragmatiki.

↓

Utambuzi wa maana iliyodhamiriwa

Usemi wowote huwasilishwa na ishara ambayo mzawa lugha hiyo (msikilizaji), anafaa kuielewa kwa kusaidiwa na muundo na mfumo lugha, ili kuelewa maana kisemantiki katika usemi huo. Ikiwa usemi utakuwa nje ya mkutadha, basi maana haitapatikana kipragmatiki. Ili msikilizaji atambue kile msemaji alinuia kusema, ataipa jukumu akili yake ili kupata uhusiano wa kile kilichosemwa, kwa kukiweka katika muktadha na ufahamu wa awali. Ufasiri wa semi huongozwa na kanuni za uhusiano - kwamba ufasiri wenyewe hufuata njia isiyo na gharama ya juu na mchakato wa kupata uhusiano hukoma pale matarajio ya msikilizaji huafikiwa au hukosa kuafikiwa.

### 1.8.3 Eksiplekecha

Ni chukulizi zinazowasilishwa na tamko katika mazingira ya kiisimu. Tamko huwa na maana wazi wakati linaendeleza umbo la kiisimu lililosimbwa la tamko au sehemu ya sentensi iliyo katika umbo mantiki (Cartson 2002). Eksiplekecha husababishwa na usimbuaji pamoja na utajirishaji wa ujumbe kisemantiki

### 1.8.4 Implekecha

Maana ya implekecha hufafanuliwa kama umbo mantiki ambalo kwa upekee wake linatokana na uwezeshaji wa maana kimuktadha. Kulingana na Cartson (2002:377), preposisheni inayowasilishwa na tamko ambalo si wazi huwa na maana fiche. Cartson anafafanua maana fiche (implekecha) kama chukulizi zinazowasilishwa na msemaji ambazo huzalika kupitia urejeleo wa mchakato ya kipragmatiki. Aliongeza kuwa yaliyoko kwenye dhana fiche huletwa na urejelezi wa kipragmatiki. Implekecha huhusisha urejelezi.

### 1.8.5 Pragmatiki leksika

Pragmatiki hujihusisha na maana katika muktadha, masuala ya mawasiliano na ufasiri wa ujumbe. Katika pragmatiki leksika maana halisi ya neno huweza kuathiriwa na muktadha wa matumizi. Kwa mfano, muktadha ambamo neno hutokea katika methali za sitiari hutokea haiwezi kudumishwa. Maana halisi ya neno huathiriwa, hivyo, kupata maana tofauti na ile ya kiisimu

Mtazamo wa pragmatiki leksika huwa na viwango viwili vya kuchunguza leksemu: kiwango cha kisemantiki leksika na kiwango cha maana kimazungumzo. Katika kiwango cha kisemantiki leksika, mtazamo wa pragmatiki leksika hujikita kwenye maana halisi ya neno. Inaweza pia kueleza maana ya mkusanyiko wa maneno yanayoleta maana kwa pamoja kama vile maneno ya nahau (Kidusu 2010).

Maana kimazungumzo hurejelea uhusiano baina ya kile kilichosemwa na kile kinachomaanishwa katika mazungumzo. Grice (1991) alisema kuwa maana kimazungumzo haihusishwi na kauli

yoyote bali hurejelewa kwa kutumia tamko fulani katika muktadha. Hivyo, maana ya neno uundwa kipragmatiki hili iingiliane na muktadha. Hali hii husababisha maana ya halisi kutofautiana na ile ya kimutadha.

### 1.8.6 Pragmatiki leksika na nadharia ya uhusiano

Pragmatiki leksika katika nadharia ya uhusiano iliundwa na Wilson na Sperber (2002) na Cartson (2000). Nadharia ya pragmatiki leksika ni muhimu sana katika kueleza kinachokumba leksimu na kuisababisha kubadilisha maana halisi. Wilson na Sperber (2003:282), walisema kuwa nadharia ya uhusiano na ile ya pragmatiki leksika, zinaletwa pamoja katika uchakataji na utafutaji wa uhusiano, yaani mchakato wa kipragmatiki leksika unaanzishwa na nia ya kutafuta uhusiano. Uhusiano hutafutwa kwa kufuata utaratibu wenye uwezo finyu, katika ubadilishaji jozi wa muktadha halisi na athari za kiutambuzi, kisha kukoma ama maana ipatikanapo, ikosekanapo au iridhishapo. Uhusiano uafikiwa kwa kuchakata pembejeo katika miktadha iliopo ya uchukulizi. Uchakataji wa pembejeo unahitaji kuwepo kwa uhusishaji wa vitu kama: mtazamo, kumbukizi na urejelezi na uwezo wa kuhusisha.

Tofauti kati ya nadharia hizi ni kuwa, nadharia ya uhusiano ina mchango mkubwa katika kueleza mchakato wa pragmatiki leksika, ambapo mfasiri huweza kukisia, kupanua, kubana maana za neno kutegemea muktadha linamotumika kwa kuegemea uhusiano na ufahamu wake na mkutadha linamotumika. Cartson (2007) alidai kuwa nadharia hii hutazama ubanaji na upanuaji wa maana kama mchakato inayotegemea kanuni za uhusiano- kwamba uhusiano ni chombo muhimu sana katika mawasiliano ambacho akili tambuzi hutumia ili kufasiri ujumbe unaowakilishwa. Ufasiri huu hutokea kwenye muktadha. Muktadha huo huziba pengo kati ya kinachosemwa na kinachowakilishwa.

Nadharia ya Uhusiano inasaidia katika uchakataji wa pragmatiki leksika ili kujibu maswali yafuatayo:

a. Ni nini kinachochea upanuaji na ubanaji?
b. Ni kwa nini maana kisemantiki hutofautiana na maana inayowasilishwa?
c. Ni nini kinachosababisha mwelekeo ambao ufasiri huchukua?
d. Ni mambo yepi yanayotokea katika mchakato huo
e. Ni nini kinachochochea michakato hiyo ya ubanaji na upanukaji

Cartson (2007) alidai kuwa sitiari ni mojawapo ya semi zinazohusishwa na upanuzi wa maana, kwamba upanuzi huo unahusishwa na ukiukaji mkubwa wa maana iliyosimbwa katika neno. Pragmatiki leksika inajishughulisha na: ubanaji, Upanuaji, Ukadiriaji, Upanuaji wa sitiari, Kutilia chuku (Haipabole), Uundaji upya wa neno au kirai (Uneolojia), Upanuzi wa kikategoria

#### 1.8.6.1 Ubanaji

Sperber & Wilson (2004) walieleza ubanaji wa leksika kama hali ya kufinya maana ya neno na kusababisha hali ambapo neno lenye maana pana kiisimu linatumika kwa lengo maalum. Ubanaji hufunga matumizi ya neno kiisimu na huzidisha umaanisho kwa sababu mfasiri anafaa abane fasiri yake hadi iridhishe matarajio ya uhusiano. Kwa mfano neno kunywa katika lugha ya kingereza na lugha nyingi za Kibantu linatumiwa kirejelea hali ya kulewa wala si hali ya kumeza kitu kama vile maji, chai au kitu chochote kiowevu.

#### 1.8.6.2 Upanuaji

Katika upanuaji, neno huwa na maana pana kuliko ile iliyosimbwa. Upanuaji wa leksika husababishwa na utafutaji wa uhusiano ambao huhusu uundaji wa dhana maalum ya kihali kwa msingi ya ujumbe unaopatikana katika data za enisaiklopedia za dhana iliyosimbwa. Kulingana na Wilson (2006), upanuaji wa kileksika unafafanuliwa kama hali ambapo neno hutumika kuwasilisha fahiwa za jumla kuliko maana yake iliyosimbwa, hivyo, kupanua maana kiisimu ya dhana fulani. Upanuzi unaweza kuwa wa aina mbalimbali kama vile chuku au upanuaji wa kisitiari. Upanuaji wa kisitiari hukubali dhana iliyowasilishwa kuwa na maana iliyo mbali sana na maana ya kiisimu, yaani ni usemi wa kitamathali ambao hauchuliwi kijuujuu ili kufasiriwa.

### 1.8.7 Dhana maalum ya kihali na uhusiano

Kwa mtazamo wa kipragmatiki, uhusiano unaendeleza dhana kuwa uelewa wa tamko huchukua mchakato wa sifa maalum ya kihali, hivyo, dhana inayopatikana baadaye, inaweza kuwa finyu au pana kuliko dhana leksika. Kulingana na nadharia ya uhusiano, dhana ambayo imesimbwa kiisimu katika neno huonekana kama kituo cha kufikia safu za sifa za kiensaiklopedia ambazo msikilizaji anastahili kuchagua sifa iliyo na uhusiano zaidi. Dhana hii hudai kuwa wakati wa kuchakata neno, ujuzi wa kiensaiklopedia huchochewa na uhusishaji wa neno/tamko na muktadha ili fasiri ya tamko lililotolewa ipatikane.

Sperber alibaini kuwa, uundaji endelevu wa dhana maalum ya kihali katika msingi ya uhusiano, unaweza kusababisha ishara ambayo upanuzi wake utahusisha vipashio ambavyo havipo katika umaanisho wa dhana leksika. Kwa hivyo, dhana hiyo inaweza kuwa pana kuliko ile iliyosimbwa. Kipragmatiki, dhana maalum ya kihali inachukuliwa kama kipande cha proposisheni ya kile msemaji ananuia kukisema katika hali fulani; ingawa wakati mwingine yasemwayo yanaweza kukosa maana iliyosimbiwa.

Umaanisho wa ishara ya sitiari, unaweza kuhusiana sana au kwa karibu na maana halisi ya maana iliyosimbwa. Mtazamo fahamishi wa nadharia ya uhusiano huunganisha tofauti kati ya maana za neno na matumizi yake na uwezo wa kiutambuzi ili kuunda dhana maalum ya kihali. Dhana maalum ya kihali ni muhimu wakati maana ya kiisimu ya dhana iliyotajwa hahitimishi matarajio ya uhusiano. Dhana hii inaleta maana ambayo ni tofauri kidogo na maana iliyosimbwa ya neno fulani. Tunaweza kusema kuwa maana za kileksika ni mianzo ya kurejelea kwani dhana inayoelezwa kwa kutumia maneno inaweza kufafanuliwa zaidi kuliko ilivyosimbuliwa.

Kulingana na Blackmore (1992); matamshi huwa kianzo kinachohitaji kutajirishwa ili kiwe kiwakilishi kamili cha akili. Aidha, yanaweza kutajirishwa kupitia mchakato wa eksiplekecha au kupitia mchakato rejeleo wa implekecha, ambapo, anachonuia kusema msemaji huwa ni pana sana na hufichika katika kile kinachosemwa. Maana kiisimu hueleza moja kwa moja yale anayojaribu kusema msemaji. Msemaji huchunguza kanuni za kipragmatiki ili kuunganisha mwanya kwa kumrejea msikilizaji kwa kanuni zizo hizo ili kufasiri tamko. (Horn 2004: 4).

## 1.9 Mbinu za utafiti

### 1.9.1 Ukusanyaji wa Data.

Mtafiti alikusanya data kwenye maktaba. Data iliyopatikana kutoka kwenye vitabu vya methali na pamoja na vitabu vingine vya marejeleo ilimfaa sana mtafiti katika kazi yake. Baada ya vitabu kusomwa, methali za sitiari zilitafutwa kwa msingi wa muundo ambapo methali zilizo muundo wa kulinganisha wa dhana au kirai na kingine kwa njia ya moja kwa moja ziliteuliwa. Mtafiti alilenga sitiari zenye leksimu moja au kirai kutoka kwa kamusi hasa kamusi ya Kitula na Ndalu (1989) na Mkota, A. (2009)

Katika methali, kuna falsafa mbalimbali kama vile; uadilifu, itikadi, uongozi na ushauri. Mtafiti alisoma vitabu hivi na kuchunguza kila methali kwa lengo la kubainisha sitiari iliyoko ili kuichunguza kwa lengo la kubaini namna mahusiano ya dhana ya sitiari huchangia kuibua fahiwa za maana na kukuza falsafa katika sitiari husika. Katika kufasiri ujumbe, mchakato wa ufasiri ulitegemea muktadha wa matumizi ya methali nzima katika ulimwengu halisi pamoja na lengo la msemaji la kutumia methali husika.

### 1.9.2 Sampuli ya data

Kwa kujikita katika muundo pamoja na dhana inachorejelewa katika methali, tulipata sampuli nyingi za methali za sitiari dhanifu kutoka kwa kamusi za methali. Kutokana na wingi sampuli, tuliainisha methali katika vikundi viwili ambavyo ni: sitiari zenye muundo kirai na sitiari za leksimu moja, ambazo pia tuliziainisha katika vikundi viwili ambavyo ni: sitiari zinazorejelea leksimu dhahania na vifaa halisi.  Baadaye, tulichagua methali chache kutoka kwa kila kikundi kwa bahati nasibu. Dhana zilizorejelea kifaa dhanifu, kifaa halisi  na  zinazorejelewa  wa kirai

ziliteuliwa na kuchunguza ama namna mahusiano ya dhana hizo huzua maana mpya au namna dhana moja hueleweka kwa msingi ya dhana nyingine. Ulinganishi huu ulihusisha sifa za dhana/ istlahi moja kulinganishwa dhana na nyingine katika kiwango cha leksimu au kirai. Ili kutekeleza mahitaji ya tasnifu hii, sitiari ziliainishwa kwa msingi ya muundo na mchanganuzi alijikita katika ulinganifu wa leksimu/dhana chanzi (DC), ambayo sifa zake ndizo nguzo kuu katika mahusiano hayo, yaani sifa hizi ndizo hutumika kama sitiari katika methali na ndizo "zinazochotwa" na kuhamishiwa dhana lengwa (DL).  Kwa msingi ya dhana maalum ya kihali sifa za DC ziliwasilishwa na leksimu kwa msingi ya vitomeo vya ensaiklopedia ili kupata sampuli ya sifa za leksimu husika. Kisha DC ilichunguzwa kwa msingi ya kufanana kwa sifa za dhana ya pili DL ili kupata maana inayokusudiwa na msemaji au mtumiaji wa methali kwa kulinganisha dhana husika.

### 1.9.3 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data, ulielekezwa kwa methali za sitiari dhanifu. Data iliyopatikana ilitegemea sifa za kiensaiklopidea za leksimu iliyotumika kama sitiari katika methali, aidha, mahusiano ya maana ya leksimu husika pamoja na muktadha wa matumizi ulitumika. Kwa kuangalia muundo wa methali, ilikuwa rahisi kubainisha DC na DL.  Mtafiti alichunguza na kuchanganua sitiari, kufuatana msingi ya nadharia ya uhusiano, na malengo thabiti ya utafiti wake, kwa kujifunga katika upeo wa utafiti wake. Alitambulisha aina za ishara za dhana na kuorodhesha sifa za ensaiklopedia za DC, mwishowe, tulionyesha namna sifa hizo huteuliwa moja kwa moja na mchakato wa kiakili unaofuatwa hadi maana ipatikane.

# SURA YA PILI

## AINA ZA METHALI NA SITIARI

### 2.0 Utangulizi

Dhana zinazorejelewa katika methali ni nyingi na hutumiwa ili kurejelea hali, tabia na sifa mbalimbali za mtu au kitu. Dhana hizi hupangwa kwa utaratibu fulani wa kisintaksia na hutumika kwa kusudi la kuwasiliana. Mpangilio wa dhana unaweza kuzua aina mbalimbali za maana ambazo zinaweza kuzua misingi mbalimbali ya kuainishia methali. Kama vile uainishaji kulingana na maudhui, dhamira na mtindo. Uainishaji kulingana na mtindo unaweza kuzua mtindo wa kibalagha, kitashibihi, chuku na kimetominia.

Sifa moja miongoni mwa sifa zingine za methali ni kuwepo kwa sitiari. Maneno yaliyotumika katika methali hutumika kitamathali, hivyo, maana yake huhitaji kufasiriwa kwa makini. Utafiti wetu unalenga kuchunguza namna neno hupata maana mpya na kuweza kufafanua neno lingine haswa linapotumika katika methali za sitiari. Kabla ya uchunguzi huu ni vizuri kubainisha methali tutakazojikita kwacho katika utafiti huu.

### 2.1 Uainishaji wa methali

Dabaghi et al. (2012) na Mkota (2009) waliainisha methali kwa msingi ya ishara inayopatikana katika matumizi ya methali. Alisema kuwa ishara za methali zinaweza kuwa za kisenedoki/ taashira, kisitiari, chuku au paradoksi au kitashibihi.

#### 2.1.1 Methali za kisinedoki

Methali za kisenedoki ni methali ambazo hutumiwa kitaashira. Taashira ni tamathali ambapo jina au neno linahusishwa na kitu au mtu linatumiwa badala ya mtu huyo au kitu hicho. Methali za aina hii zinarejelea kitu kamili kwa kutaja sehemu ya kitu hicho. Kama vile:

*Siku njema huonekana **asubuhi***

***Kidole** chema huvikwa pete*

*Ajabu ya **shingo** kukataa kulala.*

*Mtegemea **nundu** haachi kunona*

### 2.1.2. Methali za sitiari za kimetonimia

Ni sitiari zilizo na msingi yake katika mahusiano baina ya vitu viwili au zaidi vilivyotajwa ambapo kinachotajwa kina uhusiano na kinachomaanishwa.

> *Mwenye* ***macho*** *hambiliwi tazama.* Neno *macho* limetumika kimetonimia kurejelea *Kuona*
>
> ***Damu*** *ni nzito kuliko maji.* Neno ***damu*** limetumika kurejelea ukoo au unasaba

### 2.1.3 Methali za chuku

Chuku ni mbinu ya kuongeza sifa kwa kitu au mtu fulani. Sifa hizi zinaweza kuwa nzuri au mbaya.

Mfano wa methali chuku ni pamoja na:

> *Usipoziba* ***ufa*** *utajenga* ***ukuta***
>
> *Mzigo wa* ***mwenzio*** *ni kanda la usufi*
>
> *Bahati ya mwenzio usiilalie mlango wazi*

### 2.1.4 Methali za paradoksia

Methali za paradoksia ni methali ambazo hukinzana wakati wa kuzifasiri kwa msingi wa kimaantiki. Kimsingi kinachosemwa kinaonekana kukinzana kijuujuu lakini kinapochunguzwa kwa makini kinaonyesha ukweli fulani. Mfano wa methali za kweli kinzani ni pamoja na:

> *Kufa kwa wengi ni harusi*
> *Kupotea njia ndiko kujua njia*
> *Mkono usioweza kuukata ubusu*
> *Adui mpende*
> *Ndugu wakigombana chukua jembe ukalime, wakipatana chukua kapu ukavune.*

### 2.1.5. Methali za kitashibihi

Methali za kitashibihi ni methali ambazo hulinganisha dhana moja na nyingine kwa njia ya moja kwa moja kwa kutumia maneno ya kiulinganishi kama vile: kama, ja, mfano wa, -fanana na, na maneno mengineyo ya kiulinganishi. Ulinganifu wa kitashibihi ni rahisi sana kueleweka kwa

sababu hujihusisha na maana halisi ya neno. Mfano wa methali za Kiswahili zenye ulinganifu wa kitashibihi ni kama vile:

*Maneno ni kama fumo, yakitoka hayarudi.*
*Mwanamke ni kama maji ya dafu, hayapendezi ila dafuni mwake.*
*Mgeni ni kama kengewa, huruka apendapo*
*Kawaida ni kama sheria*
*Usilolijua ni kama usiku wa giza*

### 2.1.6 Methali za kisitiari

Methali za aina hii ulinganisha neno moja na lingine bila kutumia maneno kama: ja, mfano wa, sawa na, kama na mengineyo. Hivyo, wazo/dhana au istilahi moja hueleweka na hujulikana kupitia dhana nyingine kwa msingi ya dhana/wazo au istilahi nyingine. Kupitia kwa mahusiano haya, neno moja hufanywa kuwa sitiari. Kijisehemu cha methali au sifa za dhana moja huhusishwa na dhana nyingine.

*Mgeni ni kuku mweupe*
*Msafiri ni aliye pwani*
*Cheo ni dhamana*

Sitiari za aina hii pia zinaitwa sitiari dhanifu (Lakoff na Johnson 1980). Utafiti wetu ulijikita katika sitiari za aina hii. Sitiari za aina hii hutambuliwa kupitia kwa muundo. Muundo ni sehemu muhimu inayoeleza umbo la sitiari, hivyo, ulichangia katika kupata aina za sitiari ambazo zinalinganisha dhana moja au zaidi na nyingine kwa njia ya moja kwa moja. Methali za kisitiari zinaweza kuwa katika kiwango cha leksimu au cha kirai.

## 2.2 Historia na maendeleo ya fasiri za sitiari

Ni muhimu kuchunguza namna sitiari ilikua na kuendelea ili kubaini msingi na mitazamo ya watalamu mbalimbali kuhusu sitiari. Sitiari ni dhana ya kale, ilikuwepo wakati wa Plato, Aristotle na Shakespare. Imezidi kujadiliwa, kukuzwa na kuendelezwa na wataalamu mbalimbali katika vipindi tofauti za kihistoria. Kulingana na Cruse (2000), neno sitiari linatokana na neno la Kigiriki *metaphora* linalomaanisha *uhamishaji*. Tutajadili historia ya sitiari kwa mujibu wa Cruse (2000). Cruse ananukuu mawazo ya Aristotle anasema kuwa, Aristotle alidai kuwa msingi ya sitiari huhusu uhamishaji wa maana ya kauli au neno moja hadi lingine. Kwake Aristotle, maana kisitiari ilihusu kuhamisha maana halisi ya neno kutoka maana ya kawaida hadi nyingine kwa msingi ya kufanana kwa sifa fulani za dhana hizo. Mtazamo wa Arisitotle kuhusu sitiari ni kuwa sitiari huundwa katika msingi ya kufanana kwa dhana zinazolinganishwa.

Johnson (1980, 1999) ni mtaalamu mwingine katika uwanja huu aliyechangia katika kuendeleza na kukuza sitiari. Mtaalamu huyu alibainisha kuwa sitiari ina sifa zisizopatana na uhalisi wa kawaida wa kufasiri maana ya tamko. Alifafanua sitiari kama wazo anuai linalofunganika na masuala kadha. Misingi yake ya uainishaji ilihusu sifa za kisemantiki, ambazo baadaye, zilionekana kutatiza haswa jukumu la kisemantiki katika “uwanja” wa maana ya sitiari linapochunguzwa.

Richard (1937) ni mtaalamu mwingine aliyehusika na maana na ufasiri wa sitiari, anasifiwa kwa kuleta msukumo fulani kuhusu uchunguzi wa sitiari. Alibainisha sifa za sitiari kwa kuonyesha kuwa katika sitiari kuna: kifaa kinachotumika kisitiari, maana kisitiari ya kifaa na msingi kupanulia sitiari. Ufafanuzi wa Richard ulilenga kudhihirisha kuwa kuna uhusiano baina ya kifaa kilichotumika kisitiari na maana kisitiari. Ingawa mtaalamu huyu hakudhibitisha ni vipi mahusiano baina ya dhana hizi hutokea, alipinga madai ya Arisitotle kuwa sitiari zinaweza kutafasiriwa katika kiwango cha maana ya kawaida ya neno huku akibainisha kuwa kuna mahusiano baina ya dhana husika ambayo hayawezi kuzua maana halisi ya neno husika.

Hass (1935) akinukuliwa na Cruse (2000) alisema kuwa maana ya neno huzua “uwanja wa kisemantiki” uwanja huu wa kisemantiki” huwa ni maana zote za kimiktadha za neno zilizopangwa kwa misingi ya ukawaida ambapo muktadha ulio wa kawaida zaidi unaunda msingi mkuu katika uwanja huo, nayo miktadha mingine ikijika “upandeupande”. Maana ya kisemantiki

inahusu misamiati yote na athari za kila msamiati kwa maana husika. Alithibitisha kuwa, wakati maneno mawili yanahusiana, uwanja mpya wa kisemantiki huundwa, ambapo msingi wa maana huwa muktadha unaosababisha ukuaji upya wa maana. Maana hii huitwa maana kisitiari. Mfano

***Mguu* wa kitanda**.

Cruse (2002) anasema kuwa unaposema *mguu:* unahamisha maana halisi ya neno *mguu* kutoka muktadha wake wa kawaida wa kurejelea mguu wa mtu, mnyama hadi kwa muktadha mpya wa meza. Hivyo, inafaa kutafuta sifa za miguu kutoka muktadha wa kawaida huku tukiondoa sifa zile ambazo hazina maana katika muktadha ambao neno *mguu* limetumika. Kwa misingi hii tutapata kuwa *mguu* usimamisha kitu, hutilia nguvu kitu, unaweza vunjika au kukatwa. Hivyo neno ili linapata maana.

Kulingana na Hass (1935), ufafanuzi wa sitiari ni sawa na uchunguzi wa sifa za kisemantiki ambapo sifa zisizo za kawaida zinatenganishwa na zile zilizoundwa na tamko, hivyo, sifa zenye mahusiano na tamko zinaunda sehemu ya matokeo ya kauli inayopatikana. Alidai kuwa sitiari huacha urejelezi wa mawazo, mafikira ya kibinafsi na nia iliyofichika na kurejelea kwa jumla muktadha ambapo neno hutokea. Mawazo ya Hass yamekuwa na athari kubwa katika maendeleo ya nadharia ya sitiari. Mtazamo wake Hass ni kuwa utendaji wa sitiari huhusu ubashiri wa seti za maana kimahusiano haswa maana, inayotokana na sifa za dhana moja yaani (dhana ya pili) kwa msingi ya dhana nyingine (dhana ya kwanza).

Mfano. **Juma ni simba**

Katika mfano huu, dhana msingi hapa ni *juma* na dhana ya pili ni *simba,* Hass alibainisha kuwa uhusiano wa sifa humo akilini wa msemaji au msikilizaji, hivyo umaanisho wa kimahusiano wa dhana ya pili (*simba)* unaweza kuwa kama ifuatavyo

*a)* *Mnyama hatari*
*b)* *Mnyama hodari*
*c)* *Shujaa*

Sitiari hufanya kazi kupitia kuwekelea umaanisho dhana ya kwanza (Juma). Black (1990) alisema kuwa si muhimu kwa dhana zote mbili kuhusishwa na umaanisho kwani umaanisho wa dhana zote mbili unaweza kuleta uchangamano kwa dhana ya pili (simba).

Kwa mujibu wa Cruse (2000), Sperber na Wilson (1995) walidai kuwa sitiari na tamathali zingine za lugha huwa na athari maalum ambazo huhitaji ujumbe hupeanwe hufasiriwe, huchunguzwe, huchakatwe hadi uhusiano wa kiwango kikubwa cha maana utakapopatikana.

## 2.3 Uainishaji wa sitiari

Sitiari zinaweza kuainishwa kwa msingi ya Sperber na Wilson (1995), Lakoff na Johnson (1980) na Shelestiuk (2006).

### 2.3.1 Uainishaji wa sitiari kulingana na Sperber na Wilson

Wilson na Sperber (1995) waliainisha sitiari kwa kujikita katika kiwango cha ufasiriaji. Ufasiri wa sitiari hufanyika katika viwango viwili ama kiwango cha leksimu au kiwango cha kirai, kishazi au sentensi.

#### *2.3.1.1 Sitiari huru*

Sitiari huru ni sitiari zinazofasiriwa katika kiwango cha leksimu. Ricor (1997:9), anafafanua sentensi ya sitiari kama sentensi ambayo inalinganisha kitu/vitu kwa kitu/vitu vya aina mbalimbali kwa msingi ya neno moja.

Mfano wa sitiari huru*: Johana ni* ***nyumbu***

Maana ya sitiari huru hupatikana katika data za enisaiklopedia ikiwa na chukulizi moja au zaidi ambazo zimeitamalaki na zinazoweza kuafikiwa kwa hali ya juu. Unaposema kuwa Johana ni *nyumbu* itamaanisha kuwa Johana ni *mkaidi* kwa sababu sifa moja ya nyumbu ni ukaidi. Sitiari za aina hii hutumiwa na msemaji asiyetaka kusema mambo yake kwa njia ya moja kwa moja, hivyo hutumia ishara na kutoa kauli isiyo ya moja kwa moja inayohitaji kudhibitishwa.

#### *2.3.1.2 Sitiari funge*

Sitiari funge ni sitiari ambayo fasiri yake hupatikana katika kiwango cha kirai, kishazi au sentensi kwa jumla. Kulingana na Sperber na Wilson (1995) msemaji au msikilizaji anaweza kuvuka mipaka ya kuchunguza muktadha wa karibu pamoja na sifa za dhana zinazohusika, yaani anaweza akachunguza mipaka mipana kwa kujitwika jukumu kubwa la kuangalia namna kauli fulani imetumika ili aibuke na maana pana za kauli hiyo.

Uainishaji wa Sperber na Wilson (1995) ndio uainishaji unaojishughulisha na uhusiano pamoja athari za kimuktadha kwa neno. Hivyo utatupatia nuru katika utafiti wetu wakati wa kutafuta maana na kuchunguza namna sitiari zinavyoweza kufasiriwa halkadhalika namna dhana hupata maana kupitia kwa dhana nyingine.

### 2.3.2 Uainishaji kulingana na Johnson na Lakoff

Uainishaji kulingana na Lakoff na Johnson (1990) uliibuka na aina zifuatazo za sitiari: sitiari za msimbo wa ishara (konduiti), sitiari za kihali/kimaeneo, sitiari za kiontolojia

#### *2.3.2.1 Sitiari za kiishara (Konduiti)*

Ni namna ya kuwasiliana kwa msimbo. Katika mtazamo huu, msemaji husimba mafikira yao halafu anayawasilisha kwa hadhira/wasikilizaji, nao msikilizaji/wasikilizaji huupata ujumbe uliosimbwa na kuusimbua ili kuifikia maana iliyokusudiwa (Redd 1979: 285). Utaratibu huu unaonekana kufuata mkondo ufuatao:

Nia ya msemaji → ujumbe kutafakariwa kimuktadha → kusimba kutuma → ujumbe uliotumwa kusimbuliwa → ujumbe kutafakariwa kimuktadha → fikira au nia ya msemaji kuafikia.

Mfano wa sitiari ambapo dhana moja hujengwa kwa msingi ya dhana ingine:

*Nilikupa* ushauri huo
Neno hili *limebeba* maana ndogo

Kulingana na Lakoff na Johnson (1980:11), aina nyingi za virai hivi, huangazia njia za kawaida za kuwasiliana kupitia kwa lugha za binadamu. Hivyo, hazitoi ufafanuzi sana kuhusu aina za tamko zipatikanazo katika lugha za kila siku.

#### *2.3.2.2 Sitiari za kioriento*

Sitiari za aina hii hazijaundika kwa misingi ya dhana zingine ila hupanga mfumo mzima wa kidhana kwa msingi ya mahusiano baina ya dhana hizo. Neno la kisitiari linatokana na ukweli

kuwa sitiari hizo zinahusiana kwa kiwango kikubwa na hali au mahali. Sitiari zinahusu/hurejelea mpangilio wa ishara kama vile nyuma mbele, juu-chini, mashariki- magharibi na ishara zinginezo za aina hii (Johnson na Lakoff 1980). Sitiari za aina hii katika lugha ya binadamu ni asilia kwa sababu ya hali ya kitamaduni na ya kimaumbile, hivyo, hali kama hizo za kioriento si dhahania. Mfano

*Furaha ni juu, huzuni ni chini*
*Tamaa mbele mauti nyuma.*
*Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.*

#### *2.3.2.3 Sitiari za kiontolojia*

Zinaunganisha tajriba ya mtu na vifaa; kama vile miili yetu, mtazamo ya mawazo, matukio, hisia na matendo ya kidutu au vitu dhabiti (Johnson 1980). Uainishaji wa aina hii huwapa watu njia mbadala ya kutazama matukio, vitendo, mhemko, mawazo kama vidutu au vitu dhabiti. Ni njia msingi ya kutazamia vitu tunayofahamu ambavyo ni vya kidhahania vinavyopatikana katika mazingira yetu. Aina hizi za sitiari ni nyingi katika lugha mbalimbali na huwa na majukumu mengi.

*Dunia mwendo wa ngisi, kiumbe siuleme*

### 2.3.3 Uainishaji wa sitiari kulingana na Shelestiuk

Shelestiuk (2006) katika juzuu lake alibainisha kuwa sitiari zinaweza kuainishwa kwa misingi wa kisemantiki, kipragmatiki na kimuundo. Uainishaji wake Shelestiuk ulihusisha kiwango kipana cha lugha kushughulikia sitiari, haswa viwango vilivyo na mchango mkuu katika lugha na maana. Uainishaji wake kuchukua mikondo sintaksia, pragmatiki na semantiki.

#### *2.3.3.1 Uainishaji kiuamilifu*

Kwa mujibu wa Shelestiuk (2006), uainishaji wa kiuamilifu ulipendekezwa na Arutyunova (1975). Mtalamu huyu, anadai kuwa uainishaji wa aina hii unatokana na uainishaji wa dhana ya neno wa Morris (eds). Morris aliainisha neno mara mbili, akasema kuwa kuna neno lililo na jukumu la kubainisha na kuarifu. Uainishaji wa uamilifu unajikita katika chukulizi kuwa maana

kisemantiki iliyoko katika neno, inaundwa kwa msingi ya kukubaliana na jukumu lake katika matamshi. Mfano mtu anaposema *mama* jukumu la neno hilo ni *mlezi/ulezi/malezi*. Shelestiuk anaeleza kuwa jukumu la kimsingi la kimawasiliano la sentensi ni kubainisha ujumbe na kuarifu. Nayo maana ya neno kipragmatiki hujikita katika jukumu hili la kubainisha na kuarifu.

Kulingana na Arutyunova (1999) akirejelewa na Turanina (2009) alisema kuwa uainishaji wa sitiari kifasihi ujikita katika msingi ya uamilifu katika kiwango cha kujieleza kupitia kuhusiana kwa umbo na maana. Sitiari katika ulimwengu huu zinalenga kuainishwa kulingana na jukumu zinazotekeleza katika mazungummzo: kama vile kueleza dunia ni nini kwa undani, kueleza sifa za ndani za binadamu, kueleza michakato ya kihisia na halisi ya kibinadamu, kueleza matendo na mienendo ya binadamu, udhaniaji (Arutyunova (1999).

Katika misingi hii, sitiari za methali za Kiswahili zina majukumu mengi sana zaidi ya yale yaliyotajwa na Turanina (2009). Sitiari zifuatazo zinaeleza jinsi ulimwengu ulivyo na zinatumiwa kurejelea uhusiano baina ya watu na tabia za watu zinazodhihirika miongoni mwa watu:

*Asiyekosa ni malaika*
*Dunia ni mapishano*
*Dunia ni watu*

Kuna zingine zinazofafanua kuhusu sifa za ndani za binadamu

*Fadhila ni utumwa*
*Kupeana ni kikoa*

Zingine zinatekeleza majukumu ya kufafanua mchakato ya kihisia na kihalisi ya binadamu.

*Kelele nyingi ni makeke*
*Jirani ni ndugu*

Zingine zinafafanua matendo na mienendo ya binadamu

*Siasa si nanga ni tanga*
*Cheo ni dhamana*
*Tabia ni ngozi ya mwili*

Huku zingine zikifafanua mambo ya kudhania tu

*Ivushayo ni mbovu*

Suala la uamilifu au jukumu linalotekelezwa na sitiari ni dhahiri. Uamilifu wa sitiari dhanifu hunapatikana katika utajirishaji wa neno ambapo DL inabainishwa kwa msingi ya DC. Kwa kutazama mfano iliyo hapo juu, inabainika kuwa mahusiano DL na DC yanatoa mwelekeo fulani kuhusu hali, tabia, mienendo na fikira ambazo zinachangia kutekeleza majukumu fulani katika ulimwengu. Muundo uliotumika hapa ni ule wa dhana iliyo na sifa za kutekeleza jukumu fulani kulinganishwa na dhana nyingine iliyo na uwezo wa kuzua fafanuzi kuhusu hali, tabia, mienendo na mambo mengineyo. Kulingana na Shelestiuk (2006), DL inabainishwa au kusifiwa na sitiari DC.

#### *2.3.3.2 Uainishaji wa kimuundo*

Shelestiuk (2006), alisema kuwa sitiari zinaweza kuainishwa kwa kuangalia muundo wa sitiari. Kwa msingi huu inawezekana kuwa na sitiari zinazojifunga kwa ama neno, kirai, kishazi au proposisheni. Aidha uainishaji wa sitiari kimuundo, unaweza kuwa katika kiwango cha leksimu na kirai. Uainishaji huu huzua sitiari huru na sitiari funge. Kwa mujibu wa Ricour (1997), sitiari huru hupatikana katika methali na maana yake hueleweka kutoka kwa leksimu. Sitiari funge nazo hufafanuliwa kama kauli moja ya sitiari ambayo hufafanuzi wake hujikita katika mahusiano ya fungu la maneno. Kimantiki, sitiari funge hufasiriwa katika viwango vya kirai, kishazi na hata sentensi nzima.  Mfano wa methali za sitiari huru:

*a. Ahadi ni deni*
*b. Upishi ni kuni*
*c. Maisha ni mshumaa uso mkesha.*
*d. Utajiri ni raha ya leo duniani, mateso ya kesho ahera*

Kwa kuangalia sitiari ya (a) na ya (b) zilizo hapo juu, DC *deni* na *kuni* ambazo ni leksimu, zinatoa sifa zinazofafanua DL yaani *ahadi* na *upishi* mtawalia. Kinyume na methali ya (c) na ya (d) ambapo maana ya DC inapatikana katika umbo la kirai; *mshumaa uso mkesha* na *ni raha ya leo duniani na mateso ya kesho ahera*. Virai hivi ndivyo vinafafanua/ au kutoa sifa ya DL ambayo ni *maisha*, na *utajiri* mtawalia. Sitiari ya (c) na (d) ni sitiari funge kwani maana yake inafaa ijikite kwa maelezo ya ufafanuzi. Sitiari funge huwa na maneno ya ziada ya kuzieleza

sitiari awali. Huweza kuwa katika kiwango cha kishazi au kirai. Tazama muundo wa methali (c) na (d) hapo juu.

Uainishaji wa kimuundo pia unaweza kuchukua misingi ya uainishaji unaoitwa *Brocke-Rose* ambao unajikita katika aina za maneno na mpangilio wa maneno. Shelestiuk (2006) anasema kuwa mkondo huu unaweza kuwa na muundo wa sitiari kama vile *DC ni DL* au DC inabadilika na kuwa DL. Aidha kwa kuangalia aina za maneno tunaweza kuwa na sitiari za nomino, kivumishi na kitenzi. Mfano ya sitiari zilizo na muundo wa DC ni DL zinaweza kupatikana katika vitengo mbalimbali vya aina za maneno. Mfano kuna methali ya sitiari iliyolinganisha kitenzi kwa kitenzi au nomino kwa nomino ni kama: *kutoa ni kujiwekea* na *pilipili ni mchanga* mtawalia. Kwa misingi hii, dhana moja inaeleweka kwa msingi ya dhana ingine.

#### *2.3.3.3 Uainishaji wa kisemantiki*

Shelestiuk (2006) alisema kuwa uainishaji wa aina hii una misingi yake katika msingi ya maana. Anasema kuwa uainishaji wa aina hii unaweza kuonekana katika hatua nne. Kwanza, kwa kuangalia msingi ya kuunganika kimahusiano kwa dhana DC na DL zinazolinganishwa. Kwa mtazamo wa maana, tutaona kuwa kuna uhusiano uliopo baina ya dhana husika ambao huweza kusababishwa na mfanano wa ama umbo, matukio au muundo wa dhana zinazolinganishwa kwa njia ya moja kwa moja (Shelestiuk 2006). Pili, uainishaji wa aina hii unaweza kufanyika kwa msingi ya maana kisarufi-mantiki ya sitiari, ambapo misingi ya kuunganika kwa DC na DL hunafafanuliwa kwa:

i. Sifa za umbo/sura/kitu kwa kupitia umbo/sura/kitu kingine,
ii. Sifa za umbo/sura/kitu kupitia kitendo
iii. Sifa za umbo/sura/kitu kupitia sifa
iv. Sifa za kitendo kupitia umbo/sura/kitu
v. Sifa za kitendo kupitia kitendo
vi. Sifa za kitendo kupitia kitendo kingine
vii. Sifa za kitendo kupitia sifa
viii. Sifa ya kusifu kupitia kwa kitendo
ix. Sifa ya kusifu kupitia kwa sifa ingine.

Shelestiuk alisema kuwa sitiari zinazotaja vitenzi vilivyonominishwa na vikalinganiswa na vitu vingine vinaeleweka kwa msingi ya maana. Uainishaji wa tatu kisemantiki ni ule unaochunguza kinachorejelewa na DL. Kinachorejelewa kinaweza kuwa sehemu, jukumu, wanyama, chakula, ndege, maua, ujuzi, samaki na virejelewa vinginevyo ambavyo hutajwa katika methali. Mwisho, uainishaji wa kisemantiki unaweza kuainishwa kwa kulirejelea udhabiti na udhahaniaji wa sitiari DC ambapo dhana ya DL inaweza kuonyesha udhabiti au udhahania wa sitiari. Udhabiti wa sitiari unatokana na utumiaji wa sifa bainifu za kisemantiki ambazo humwezesha mhakiki kupata picha fulani katika kazi ya fasihi na kuibua fahiwa fulani akilini mwake. (Murdoch 2013). Aidha, Murdoch alisema kuwa sitiari dhabiti hutumia kitu dhabiti kukilinganisha na kitu kingine kinachofanana na wazo fulani kwa njia ya muundo, matukio, umbo au udhaniaji. Anatoa mfano wa *utunzaji wa yai* kama sitiari dhabiti inayomaanisha *kumakinika sana*.

**2.4 Dhana ya sitiari dhanifu**

Dhana ya sitiari ni changamano, ina mtazamo mbalimbali ya kuifasili. Hata hivyo, baadhi ya wataalamu wanaitazama kwa namna tofauti. Black (1990, 1994:28) alisema kuwa sitiari dhanifu haina mfanano halisi wa moja kwa moja baina ya dhana zinazowekwa kwenye ulinganisho, ila inaundika katika mfanano wa sifa. Alidai kuwa kinachoonyesha kuwa kauli ni sitiari, ni ule utafutaji, usisitizaji na upangaji wa sifa za dhana msingi (DL) kwa kuichunguza kwa msingi wa dhana ya pili (DC). Maoni ya Black (1990) yanasisitiza kuwa kuna sifa fulani bainifu katika dhana zinazolinganishwa. Vilevile, katika kufasiri sitiari, Black (1990) alisisitiza kuwa hakuna uhusiano halisi sawa uliopo baina ya dhana hizi bali mfanano husababishwa na kuwepo kwa sifa za dhana husika. Aidha, viambajengo vitatu vinavyounda sitiari ambavyo ni pamoja na: dhana lengwa (*focus*), sifa (*properties*) na dhana chanzi (*frame).*

Lakoff na Johnson (1980) waliendeleza wazo la Black, wakasema kwamba sitiari ni zao la kuramani uhusiano wa sifa baina ya DC hadi DL. Kulingana na Lakoff na Johnson, (1980), sitiari dhanifu hupatikana katika kila mazungumzo. Sitiari hupanga kijozi vitu viwili ambavyo huenda havifanani kiumbo au kimuundo na kuvilinganisha. Hivyo, kitu kimoja kinasemwa ni kingine.

Shelestiuk (2006) aliangalia muundo wa sitiari kwa jumla na kudai kuwa kuna sifa maalumu zinazodhihirika. Alisema kwamba DC na DL zinaweza kutokea kwa muundo {A ni B} au {A huwa B}. Matumizi na ufasiri wa sitiari kwa jumla huwa na msingi yake katika tajriba za kimazingira na kitamaduni za jamii na inapotumiwa huwa inatoa maelezo kuhusu falsafa, mitazamo na hali za jamii. Kwa misingi hii watu huweza kuelewa sitiari kwa misingi ya kijamii na vile vile kuielewa jamii inayotumia sitiari hizo.

**2.5 Sifa za jumla za lugha ya sitiari**

Katika lugha za walimwengu sitiari imejitokeza na sifa mbalimbali. Kwanza, *sifa ya ubia*. Kulingana na Lakoff na Johnson (1980), sitiari dhanifu zinapotumiwa katika kauli, kauli hizo hujaa udhanifu wa kujieleza ambao huzalika kwa njia isiyo ya moja kwa moja na sitiari. Wataalamu hawa wanatetea kuwa lugha ya mazungumzo ya binadamu hujaa sitiari.

Blumenberg (1979) alitetea kuwa ufikiriaji wa mwanadamu ni wa kisitiari kwa sababu ya udhanifu na maelezo ya kisayansi yaliopo. Alidai kuwa kinachotumika siku baada ya siku katika kufikiri na kutenda kazi ni kanuni-bia ya lugha ambazo hufanya udhanifu kuwezekana kwa kufikiria kisitiari.

Sifa ya pili ya sitiari ni *usafu wa maelezo.* Sitiari dhanifu, hazifanyi kazi kivyake (Lakoff na Johnson, 1980). Huhusishaji wa kisitiari unaweza kutoa mfumo sawa wa ishara ya sitiari, na safu zinazofanana za maelezo ya dhana fulani. Mfano wa sitiari kama *muda* ni *pesa*. Ina maana kwamba *muda* ni *raslimali haba* au *muda* ni bidhaa *ya thamani.* Kupata sifa kama hizi ambazo zinadhihirika moja kwa moja kama sifa za pesa, kutasaidia kuelewa dhana ya muda. Usafu wa maelezo kama vile *raslimali haba*, *bidhaa ghali* zote zinaweza kutumiwa kurejelea pesa kwani pesa ina sifa kama hizi.

Sifa ya tatu ya sitiari ni *sifa ya Kutajirisha maana kisemantiki*, Sitiari katika mfumo wa kiisimu unahusu utajirishaji wa neno kwa maana mpya, kulipatia neno maana pana pamoja na kuunganisha maana inayojulikana na ile isiyojulikana. Kulingana na Johnson, uramani wa maana ya neno kisemantiki huunganishwa kwa njia ya moja kwa moja na nyingine. Semantiki tambuzi hushikilia kuwa upataji wa maana leksika mpya hufikiwa bila msingi mahsusi na una misingi

yake katika muundo wa kiutambuzi ambao ndio hufanya maana halisi ya neno kutofautiana na kuhusiana na ile nyingine kwa njia inayofaa.

Mfano neno *juu*

a. Sauti kubwa
b. Enye kutoa sauti kubwa
c. Enye kusikika kwa urahisi
d. Kilicholalia kingine
e. Alama zilizozidi
f. Bei iliyozidi ya kawaida.

**2.6 Fenomena zinazohusiana na sitiari**

Fenomena hizi zilijadiliwa na Shelestiuk (2006), mtaalamu huyu alionyesha mtazamo wake kuhusu dhana ya sitiari za kisasa, kuwepo kwake na muundo wake. Alitathimini aina mbalimbali za sitiari na kujadili fenomena husika zenye msingi-sawia katika lugha asilia. Alisema kuwa fenomena inaweza kuhamishiwa fenomena nyingine kwa msingi ya ufanano baina ya fenomena husika. Sitiari inarejelea dhana fulani ambayo inaweza kujitokeza na fenomena zifuatazo.

2.5.1 **Uhishi wa kisitiari**

Uhishi wa sitiari pia hujulikana kama prosopopeia. Fenomena hii hutokea kwa sitiari maalum, ambapo kitu au dhana dhahania hupewa sifa maarufu za kiumbe. Kwa mfano, *Dunia* kupewa *sifa za mapishano.* **Dunia** inapewa sifa za binadamu na haina uwezo wa kupisha au kupishwa. Hii ni sifa ya uhishi wa kisitiari. Uhishi wa kisitiari unaweza kuwa wa falasia la kipathetiki (*pathetic fallacy*) ambapo kuna udhaniaji wa kitu kuwa hasimu kwa binadamu. Katika uhishi wa kisitiari vilevile, kuna ritifaa (*apostrophe*). Ritifaa inahusu kuzungumza moja kwa moja na kitu ambacho katika uzungumzaji huo ufahamu hukuzwa, mfano, *jogoo analia "uta wangu uli kule".* Jogoo hana maneno kama haya, ila methali inayasawiri kama yaliyosemwa kwa njia ya moja kwa moja kwa mtu au kitu fulani. Mwisho, katika uhishi wa kisitiari, kuna wazo la udokezaji, udokezaji ni urejelezi wa kitu kinachodhaniwa kujulikana sana baina ya wazungumzaji kutoka

kwa fasihi au visasili. Mfano wa methali zenye udokezaji ni kama vile: *fadhila ni* ***Utumwa*** *au Huwi* ***Musa*** *kwa kubeba fimbo au Huwi Musa kwa kuvaa kanzu ndefu.* Neno **utumwa na Musa** hapa ni neno la kisaasili na hurejelea hisitoria za biashara za utumwa naye Musa ni mtu katika bibilia aliyewakomboa Waisraeli kutoka Misiri kwa nguvu za mwenyezi mungu mtawalia

Fenomena nyingine inayohusishwa na dhana za sitiari ni:

### 2.5.2 **Ufumbaji wa maongezi**

Ufumbaji wa maongezi ni fenomena hii hutokea baina ya uzungumzaji ambapo kitu hubandika jina la kitu kingine kwa msingi ya kufanana kwa sifa fulani, kwa kusisitizia sifa au uhusiano fulani wa dhana hizo. Matukio kamili ya sifa hii huwa ni uinuaji wa mtindo au chuku. Methali zifuatazo zina sitiari zenye sifa ya ufumbaji wa maongezi

*Mzigo wa chungu* ni *chembe moja ya mchele*

Msafiri ni *aliye pwani*

Hii ni dhana kuu katika methali kwani neno hutumiwa kwa njia inayofumbwa. Mfano, kirai *mzigo wa chungu*, linaweza kutumiwa kiufumbaji katika maongezi kuonyesha, *tatizo la maskini*. *Chembe ya mchele* kumaanisha *jambo ndogo*. Kirai *Aliye pwani* kinatumika kumaanisha *aliyejitayarisha kwa jambo kikamilifu.*

### 2.5.3 Antonomasia ya sitiari

Antonomasia ya sitiari ni matumizi na neno la kipekee la mtu mashuhuri kumtajia mtu wa kawaida. Katika methali kumejaa antonomasia za kisitiari. Mfano, *Fumo Bakari si yeye ni maina kufanana.* Neno Fumo Bakari linatumika kumrejelea mmojawapo wa mashujaa katika eneo la pwani ya Kenya. Jina hili linatumiwa kumrejelea mtu anayejisifu kuwa na sifa fulani ambazo kwa kawaida hana.

### 2.5.4 Sinesthesia

Sinesthesia ni fenomena nyingine ya sitiari ambayo hutajwa kama fenomena ya kuhamisha kitu hadi kingine kwa ufanano wa mitazamo ya kimsingi inayotokea katika nomino zinazotaja sifa za kitu au vitenzi na vivumishi. Leksimu sinesthesia za kawaida ni kama zile zinazorejelea hali ya

kuhamisha sifa za dhana halisi hadi kwa dhana halisi nyingine au kuhamisha sifa za dhana halisi hadi kwa fenomena za kihisia na kiakili. Mfano.

Dhamira **safi** ni tandiko **laini**

Katika methali hii *sifa za tandiko **laini*** zinahusishwa na *dhamira **safi***. Tandiko laini kwa misingi ya sinesthesia ni; dhana halisi nayo "dhamira safi" kwa msingi ya sinesthsia ni dhana ya kiakili. Hivyo, sifa za dhana halisi zinahamishiwa dhana ya kiakili.

### 2.5.5 Ishara za kisitiari

Ishara za kisitiari ni ishara sanisi za kiutamaduni zilizo na mfumo wa kiuteuzi ambapo usanii wa kimsingi hufanana na maana ya karibu ya dhana ya msingi, usanii wa pili wa dhana ni wa karibu sana na udhanifu wa kijumla ambao unaunganika na dhana ya kimsingi kwa ulinganifu wa sitiari. Kama vile:

i. Waridi katika lugha ya Kingereza ni ishara ya umaridadi au Pendo.

ii. Ukuta Kikwazo
Ubanaji wa uhuru.

iii. Mlima Uinuaji wa kiroho.
Ugumu

Hii ni dhihirisho kuwa, sitiari zinahusishwa kiishara na mambo mengine kwa msingi ya utamaduni. Kwa mfano, mnyama aina ya "simba" hutumiwa katika Afrika ya Mashariki kuashiria *ujasiri* ndipo pakawa na methali zinazomchora simba kama jasiri, stadi au hatari, kama vile: *Simba ni mwenda kimya, wa mayowe hana neno* na *simba ambaye ni mngwizi halii.* Methali hizi zinatuambia kuwa ni rahisi kuepuka hatari unayoiona kuliko ile usioiona. Aidha, stadi wa jambo hasemi bali matendo humtambulisha mtawalia.

## 2.6 Hitimisho

Kutokana uchunguzi wetu, ni kweli kuhitimisha kuwa muundo wa sitiari unalinganisha dhana chanzi na dhana lengwa, ambapo dhana chanzi inaweza kuwa wazo, kifaa halisi, kitendo, nomino, kitenzi au vitu vya kufikirika au maneno ya aina mbalimbali. Aidha, dhana lengwa inaweza kurejelea vitu mbalimbali kama vifaa halisi, vifaa dhahania au mchakato fulani. Ulinganifu huu unaweza kuchukua muundo wa A ni B ambapo, A na B inaweza kuwa kirai au neno ambalo lina sifa moja inayoleta mfanano baina ya dhana hizi. Suala la muundo wa sitiari limedhihirika wazi katika kila aina za uainishaji kwamba A ni B ambapo ulinganifu wa sifa ni muhimu.

Tumebaini kuwa kuna mambo mbalimbali yanayohusishwa katika uainishaji wa sitiari, kwamba kuna suala la muundo, maana na uamilifu katika neno au maneno yanayotumika kisitiari. Masuala haya yote-ya uainishaji- yanakaribiana na kuingiliana kwa ndani sana. Hata hivyo, suala kuu linalotamalaki uainishaji wa sitiari ni muundo wa sitiari.

Tumebainisha kuwa kuna fenomena na sifa zinazopatikana katika sitiari, fenomena hizi zina mchango wake katika uainishaji wa sitiari hasa uainishaji wa kimaana na kiuamilifu. Hii inaashiria kuwa uainishaji wa sitiari si suala la kuchukulia kwa urahisi bali ni suala changamano

# SURA YA TATU

# MAWASILIANO KUPITIA SITIARI DHANIFU

## 3.1 Utangulizi

Kwa mujibu wa Soi (2014), kufasiriwa kwa methali hufaa pale methali hutumika kama tamko au katika matini ambapo msikilizaji/msomaji anahitaji kuelewa maana ya tamko hilo. Methali huweza kutumika katika mawasiliano yaliyo katika maandishi au katika mazungumzo baina ya watu. Katika sura hii, tutaangalia methali za sitiari kama tamko au matini katika muktadha wa matumizi.

Aidha, tutachunguza namna maana inavyoafikiwa katika methali husika kwa kuangalia uhusiano baina ya dhana zinazolinganishwa. Zaidi ya hayo, dhana zinazolinganisha zinaweza kuwa na uhusiano bayana kwani zinaweza kuhusiana katika maana ya neno kiisimu na zikazua maana katika kiwango hicho hicho au zikawa na uhusiano ulio wa mbali ambapo maana ya juujuu si bainifu (ni ya mzunguko), hivyo zikahitaji kufikiriwa zaidi kama kundi la maneno pamoja na muktadha linapotokea, kusudi kupata maana ambayo haieleweki kwa njia ya moja kwa moja kutoka kwa leksimu husika (Nsookwa 2010). Utafiti wetu utashughulikia methali zote zikiwemo methali zenye uhusiano bainifu na uhusiano usio bainifu.

## 3.2 Dhana ya maana

Maana ni kipengele cha msingi katika lugha na katika mawasiliano. Kila kipashio cha lugha kama vile sauti, silabi, neno na sentensi kinashirikiana na kingine ili kufikia lengo kuu la mawasiliano. Hivyo, ujuzi wa ushirikiano wa vipashio vya lugha ni muhimu katika kuelewa maana inayowasilishwa na usemi au matini mbalimbali. Suala la maana ni ngumu kufafanuliwa kwa sababu neno *maana* linatumika kwa malengo na sababu mbalimbali. Vilevile dhana ya maana hutegemea mambo mbalimbali haswa mambo yanayomhusu mzungumzaji, msikilizaji, mazingira, hali inayomzingira mtu, aina ya mawasiliano na mifumo ya kijamii. Mawasiliano huhitaji ujumbe unaowasilishwa ueleweke na huwe na maana, hufanyika kwa njia nyingi, si kwa kutamka pekee, pia kwa kuona au kutumia ishara. Kwa mfano, mtu mwenye huzuni hutambuliwa kwa haraka kama anayehuzunika kwa kumtazamwa usoni wake. Aidha, honi ya gari inapopigwa huwasilisha maana kuwa dereva anaomba apishwe njia na watumiaji njia.

Kanuni za uhusiano huongoza katika kutambua kanuni za lugha. Ingawa lugha si njia ya kipekee ya kuwasilisha ujumbe, ni dhahiri kuwa lugha ni kifaa kikuu cha mwanadamu kilicho na majukumu mengi kama vile kuliwaza, kushauri, kuelimisha au kuburudisha na hutumiwa na binadamu katika kuwasiliana kwa njia rahisi. Binadamu hunufaika sana na lugha katika kuwasiliana. Kupitia hubwiaji wa kanuni na mfumo ya lugha, binadamu huwa na uwezo wa kutunga sentensi nyingi sana zisizo za kawaida. Aidha anaweza kutumia lugha kwa shughuli mbalimbali kama vile: kutunga kazi za fasihi, kuwasilisha maana kadhaa kama vile: maana husishi, maana ya umaanisho, maana ya kimaudhui, maana leksika, na maana nyinginezo.

Kwa kutegemea jamii, maana na ukweli wa maana katika tamko unaweza kuathiriwa na mambo mbalimbali kwa sababu maana hutegemea hali ya msemaji, wakati wa mazungumzo na muktadha anamozungumzia. Mfano unaposema methali *Ujanja ni mali*. Mazingira ya neno *ujanja* yanaweza kuathiri maana ya neno hili likamaanisha ama *maarifa* au *hila*. Kwa hivyo, suala la kihistoria ni muhimu katika kupata maana ya neno. Vilevile, habari tangulizi alizonazo mtu kuhusu neno au usemi zinaweza kuathiri maana ya usemi mzima.

Dhana ya maana inaweza kupatikana katika mofu. Kwa mfano, unapomwambia mtu "*ukiingia hapo uta***ki***ona".* Ataeleweka kuwa anaonywa dhidi ya kujitafutia maangamizi. Maana ya kauli hii inapatikana kutokana na matumizi ya mofu na kwa msingi ya mofu kama vile: "ki" katika neno "uta*ki*ona" na kionyeshi dhihirishi "*hapo".* Hivyo, maana ya sentensi hii inategemea habari za awali alizonazo msikilizaji. Msikilizaji ambaye si mhusika katika mawasiliano haya anaweza asipate maana inayokusudiwa kwa sababu hatakuwa na habari za awali kuhusu mofu "ki".

Maana inaweza pia kuathiriwa na mabadiliko yanayotokea lugha kama vile matumizi ya ziada ya neno fulani. Mfano, neno "kupe" au "mzee" linapata maana mpya. Mabadiliko haya yanatokana na athari za kijamii na kisiasa ambapo neno "kupe" linatumika kumaanisha "mtu mvivu" au "mtu anayeishi kwa kunyonya jasho la mtu mwingine", ilhali neno "mzee" linatumika kurejelea mtu aliye na heshima na madaraka au watu walio na elimu na staha katika jamii. Tazama methali hii

*Ujanja ni mali*. Methali hii ni mojawapo ya methali ambayo inaweza kuzua maana isiyokusudiwa na msemaji. Neno "ujanja" limebadilika maana kutoka maana ya *maarufu* hadi

kwenye maana ya *hila*. Neno ili linatumika katika methali hii ili kurejelea "umaarufu" inaweza kuchukuliwa kuwa neno "ujanja" linerejelea "hila", ikiwa itatumika katika muktadha usio na mchango unaotofautisha maana, hivyo maana ya methali hii inaweza ikakosekana na maana ingine kuzuka kinyume na aliyokusudia na msemaji.

### 3.3 Dhana ya muktadha

Dhana ya muktadha ni pana sana, fasiri zake ni nyingi. Baadhi ya wataalam wanafafanua mkutadha kwa kurejelea vipengele vya lugha vilivyotajwa hapo awali au kwa kurejelea mazingira halisi panapotumika lugha katika mawasiliano (*Dictionary of language and linguistics*. Muktadha wa mawasiliano huwa ni mazingira ambamo washiriki huwa, uhusiano baina ya washiriki wenyewe, hali au mkusanyiko wa yote kwa pamoja. Wakati wa mazungumzo ni muhimu kutiliwa maanani kwani mawasiliano huweza kuathiriwa na muktadha na mambo mengine kama vile mfumo ya kijamii, jinsi watu wanavyohusiana na kaida zinazoongoza jamii husika.

### 3.4 Miktadha katika utunzi wa methali za sitiari na chimbuko la methali

Miktadha mbalimbali hujitokeza katika kuchimbuka kwa methali. Miktadha hii hubainika waziwazi kutokana na kile kinachorejelewa na methali husika, hivyo, kinachorejelewa hukuza wazo kuu kuhusu kuchimbuka kwa sitiari. Miktadha ya chimbuko la sitiari inaweza kutokana na ama hali mbalimbali za maisha, sifa za kimaeneo, mtindo na muundo wa kitamaduni wa jamii au masuala ya kihistoria ya jamii. Ili kuelewa baadhi ya sitiari za methali ni muhimu kutilia maanani masuala ya kihali, kitamaduni, kijiografia na kihistoria ya jamii husika.

#### 3.4.1 M**uktadha wa hali**

Kutokana na tofauti mbalimbali katika maisha ya binadamu, kumekuwepo na hali mbalimbali zinazodhihirika katika maisha ya jamii. Hali hizi za maisha zimekuwa chambo cha tajriba baina ya jamii. Kwa mfano, kutokana na mahusiano na maingiliano baina ya watu wa pwani, baadhi ya hali mbalimbali zimeweza kutambuliwa na kusifiwa au kukemewa. Hivyo, methali kama vile: *upweke ni uvundo*, *mapenzi ni kikohozi*, *utajiri ni umande* zimeibuka ili kurejelea hali za maisha. Methali hizi zimeibuka na kutumika kama kauli inayokemea hali fulani zisizokubalika katika jamii kama vile hali ya kuishi pekee au kutopenda kutangamana na watu; ambayo ni kinyume na

matarajio ya jamii. Nayo methali ya pili inarejelea hali ya kupenda mtu ambayo ni vigumu kuificha. Inalinganisha mapenzi na kikohozi ambacho si rahisi kukificha. Inaonyesha jinsi hali ya kupenda inavyosawiriwa katika jamii ya wapwani. Aidha, methali ya mwisho inaonyesha namna utajiri unavyoweza kuisha na tajiri akafilisika. Hali ya umande kukauka baada ya kila alfajiri inadhihirisha namna utajiri unaweza ukaisha na tajiri akawa maskini. Methali hizi zinachimbuka katika muktadha wa hali na zinatumika kurejelea hali mbalimbali za maisha ya binadamu. Hata hivyo methali zasitiari zinaweza kutumika katika hali sawa na hizo au hali tofauti.

### 3.4.2 Muktadha wa kijografia

Methali za aina hii huzuka kutokana na imani ya watu wa pwani kuhusisha eneo fulani na tabia au sifa fulani. Methali zinapotumiwa huwa zinaonyesha na kudhihirisha barabara mambo yanayohusiana na mazingira/maeneo fulani. Hivyo, sehemu fulani za maeneo hupatiwa sifa fulani na jamii ambapo neno mahsusi hutajwa na watumizi lugha ili kurejelea sifa hizo. Hivyo, neno linalotumiwa kurejelea sehemu hizi hutumika kisitiari na hubeba imani ya jamii kuhusu eneo lililotajwa. Pili masuala ya kihistoria yalihusishwa na maeneo fulani, Hivyo, maneno yanayotaja maeneo hayo yanapotumiwa katika methali kama kisitiari, humhitaji mchanganuzi kung'amua uhusiano wa maeneo hayo pamoja na masuala yanayoambatanishwa na maeneo husika ndipo aweze kuelewa maana ya sitiari tumika. Muktadha wa kijiografia ni muhimu katika kuakisi utamaduni wa jamii na maeneo ambayo tamaduni hizi zilihusika. Aidha ujuzi wa muktadha wa kitamaduni ni muhimu katika kutafuta maana. Methali mbalimbali zinaakisi tamaduni za maeneo mbalimbali ya pwani, hivyo, ujuzi wa kuhusisha maeneo na tamaduni fulani hunasaidia katika kuelewa maana za maneno yaliyotumika kisitiari.

a) *Waswahili wa Pemba hujuana kwa vilemba*
b) *Samli ya Pemba haimpati mtu machoni.*
c) *Mpemba hatumii fimbo akiona gogo.*
d) *Ulingo wa Kwae haulindi Manda.*
e) *Hindi ndiko kwenye nguo na waendao uchi wako.*

Methali (a) inaonyesha tamaduni za watu wa eneo la Pemba kuwa wao huvaa Vilemba kama ishara ya dini yao. Kwa hivyo, wao ni rahisi kutambuana/kutambulika na watu wengine au

kujulikana. Methali (d) inaonyesha kuwa eneo la Kwale liko mbali sana na eneo la Manda, hivyo, si rahisi kuona eneo moja ukiwa katika eneo lingine. Methali hii inatumiwa kuonyesha kuwa mtu aliye mbali na mwingine hawezi kusaidiwa anapokuwa katika tabu.

Muktadha wa kijiografia unaweza kurejelea sehemu nzima ya eneo au sehemu mahsusi ya eneo fulani. Kwa mfano *Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.* Ni methali inayorejelea sehemu fulani ya pwani ambapo mkondo wa maji ya mawimbi hupakana na sehemu kavu (upwa), inaonyesha sehenu hii kama sehemu iliyo na wanyama wengi wanaoweza kutumika kama kitoweo.

### 3.4.3 Muktadha wa kitamaduni

Methali huweza kuonyesha utamaduni wa jamii hasa jamii ya wapwani kwa njia wazi kupitia lugha. Ujuzi wa tamaduni za jamii ni muhimu katika kuelewa maana ya methali. Lugha ya methali imedhihirisha tabia, mienendo, dini, imani na mwonoulimwengu wa jamii. Kwa msingi hii methali huchimbuka kutokana na tamaduni ya jamii na sitiari zake hurejelea tamaduni hizo.
Sitiari zinazodhihirika katika methali zinaweza kurejelea dini, elimu, ndoa na mwonoulimwengu wa jamii kuhusu ulimwengu.

Mfano

*Elimu ni taa gizani huzagaa.*
*Elimu ni bahari.*
*Mke ni nyumba.*
*Mke ni tabia, mme ni jaha.*
*Kafiri akufaaye, si islamu asiyekufaa.*
*Mtumikie kafiri upate mradi wako*.

Sitiari hizi zinarejelea masuala mbalimbali ya jamii kuhusu utamaduni. Zinadhihirisha namna jamii inavyoona ulimwengu na jinsi ulimwengu unavyounda jamii.

### 3.4.4 Muktadha wa kihistoria

Baadhi ya methali za Kiswahili zimechimbuka katika muktadha wa kihistoria, kisiasa na kiuchumi. Nyingi zinabainisha wazi mambo ya kihistoria kuhusu jamii ya wapwani kwa kuweka waziwazi mambo ambayo yalikuwepo kabla ya kuvumbiliwa kwa mandishi. Kwa sababu hii, masuala mbalimbali ya kihistoria ya jamii za wapwani yaliyotekelezwa na jamii hii pamoja na mifumo ya kijamii, kisiasa kiuchumi yanadhihirika. Mfano wa methali. *Washindwao ni*

*wanaume na mata yao*. Ni aina moja ya methali inayotudokezea masuala ya kihistoria kwani inatuelekeza katika masuala ya kisiasa ambapo wanaume waliokuwa wakienda vita huku wamejihami na mwishowe kushindwa au kuangamiza na maadui wao licha ya kujipanga kikamilifu. Hii ni methali ambayo inatumiwa kuwashauri waliojihami kutojigamba kwa sababu ya uwezo wao mwingi au zana nzito za vita kwani huenda wakashindwa pamoja na wingi wa uwezo au zana walizo nazo.

### 3.5 Uwasilishaji wa maana kupitia sitiari za methali


Lugha ni chombo muhimu katika mawasiliano. Kupitia kutamka au kutumia ishara za mkono, vyombo vya mawasiliano na kadhalika ujumbe hupitishwa na maana inayokusudiwa huafikiwa. Dhana ya mawasiliano si ngeni, imekuwepo tangu wakati wa babu zetu ambao waliwasiliana kupitia nyimbo, methali, ushairi, ngoma na kupiga mbiu. Zaidi ya hayo, mbinu za mawasiliano zimezidi kuvumbuliwa kama tunavyozidi kuendelea kiteknolojia na kisayansi. Kupitia kwa mbinu hizi, mawasiliano yanaweza kutekelezwa kwa kutumia simu au kwa maandishi au yakahifadhiwa kwenye kanda za redio au filamu.

Wakati wa kuwasiliana, kuna mambo matatu muhimu. Kwanza, mawasiliano yanahitaji pawepo wahusika, yaani mtumaji ujumbe na mpokeaji ujumbe. Wahusika hao wanatarajiwa waelewane. Ili kuelewana, wahusika wanafaa washiriki utamaduni moja, kwani itakuwa vigumu kwao kuelewana ikiwa mhusika mmoja hamwelewi/aelewi utamaduni wa mhusika mwenzake. Aidha, mawasiliano huhitaji ujumbe uwasilishwe. Ujumbe unafaa husimbwe na upitishwe kwa msikilizaji kwa nia fulani na kwa malengo kadha kama vile: kuonya, kuelimisha, kushauri, kuburudisha au kuelimisha hadhira. Hivyo, msikilizaji anafaa ausimbue ujumbe hadi apate maana na lengo la ujumbe huo. Mwisho, mawasiliano huhitaji lugha inayotumika ikubalike katika kutekeleza majukumu fulani, lugha inafaa ikubalike katika kutekeleza majukumu kama vile kupongeza, kushauri, kuonya, kuzindua na kuhimiza. Kwa mfano lugha ya kuwapongeza maarusi inafaa iwe na maneno yanayosawiri pongezi. Hivyo, methali inapotumiwa katika mawasiliano, inafaa ionyeshe sifa fulani zitakazochangia kupitisha ujumbe ili ueleweke na msikilizaji, uwe na maana na ufae katika kutekeleza majukumu kwa msikilizaji.

Ili kupata maana kiuamali, ni lazima maswala zaidi ya kiisimu yazingatiwe (Carton 1999), hivi kwamba, ujumbe utahusishwa na matukio ya wakati fulani katika mchakato wa kutafuta maana

inayosimbwa na mtumaji ujumbe. Kwa mfano, unapotumia methali "*upishi ni kuni* kwa mpishi, itazua maana mbalimbali kulingana na muktadha wa kutamkika kwa methali hii. Kwa mfano, ikiwa mpishi anapika na wakati huo ana kuni za kutosha katika kipindi hiki muhimu, basi maana kijuujuu ya methali hii itapitisha ujumbe ulio na maana. Hata hivyo, methali hii ikisemwa kwa mtu anayetarajia kufanya jambo fulani ilihali hajajipanga kikamilifu basi itakuwa ikimshauri kujitayarisha kikamilifu. Hivyo, maana na jukumu la methali hii imo katika muktadha, na itabidi msikilizaji aitafute kwa kuambatana na wakati wa maongezi.

**Kielelezo cha vimiliki vya mawasiliano**




***Kilelezo hiki kinajumuisha mchakato ufuataao***


Ujumbe - ni kile anachotaka msemaji kimfikie msikilizaji

Mtuma ujumbe- ni mtu anayetuma ujumbe kwa kutumia methali

Njia- ni namna au kifaa kinachotumiwa na wanaowasiliana kufikisha ujumbe

Mpokeaji ujumbe- ni msikilizaji au msomaji anayelengwa kuupata ujumbe fulani.

**Kilelezo cha ii: Nadharia na mchakato wa mawasilinao kwa mujibu wa Haris (1993)**




Kielelezo hiki kinafafanua zaidi mchakato wa mawasiliano. Katika mawasiliano kupitia kwa sitiari watumiaji lugha hutumia tajriba zao za kimazingira kutaja dhana walizozoea sana na kuzihusisha na zile zisizozoeleka. Utaratibu huu hufanyika kwa "kuchotwa" sifa za dhana fulani kutoka kwa mazingira na kuhusisha sifa hizo na dhana nyingine. Kwingineko watumiaji wa sitiari au methali katika mawasiliano huweza kubuni majina yao na kuyalinganisha na majina mengine katika uzoefu wao wa kutumia lugha. Hivyo, wanazua kauli zinaweza kuibuka kuwa msemo wa lugha ya Kiswahili. Kisa kama hiki hufanya baadhi ya kauli ya sitiari dhanifu mara nyingi kuonekana kama si methali kwa sababu ya kuzoewa katika mazungumzo.

Kwa kutumia methali katika mazungumzo, aghlabu msikilizaji hatarajiwi kutoa jibu au kwitikia chochote, kile anachokitarajia msemaji ni kueleweka kwa anachokiwasilisha kwa msikilizaji. Hivyo msikilizaji hana budi kuchanganua ujumbe ili kuipata maana ya msemaji, anapoipata maana anaweza kutoa mwitikio wake au asiutoe (ikiwa si jambo la lazima). Ikiwa atautoa mwitikio wake kwa msemaji basi atatarajiwa atunge, asimbe na awasilishe mwitikio wake kama ujumbe. Hivyo, mpokeaji/mwandishi wa ujumbe kwa wakati huu atakuwa msemaji, naye msemaji atachukua nafasi ya msikilizaji/ msomaji. Hivyo mawasiliano yataendelea kwa njia ya mduara.

### 3.5 Mawasiliano kupitia kwa sitiari dhanifu

Mawasiliano kupitia kwa semi huhitaji kufasiriwa kwa semi hizo, ufasiri wa semi hutegemea michakato ya kipragmatiki na kisemantiki (Recanti 2004). Mtaalam huyu alieleza kuwa ufasiri wa maana ya kipragmatiki, si sawa na ufasiri wa maana kiisimu, kwani ufasiri huu unajikita katika utamkaji, lengo la utamkaji, mazingira ya utamkaji na uhusiano wa wanaozungumza. Kwa mujibu wa Akmajian na wenzake (2010) waliibuka na masuala mawili kuhusu maana; wanasema kuwa kuna maana ya msemaji na maana kiisimu. Maana kiisimu ni maana kisemantiki na hufasiriwa kwa njia ya moja kwa moja. Nayo maana ya msemaji ni kile anachomaanisha mtu kwa kutamka tamko fulani. Maana hizi mbili ni tofauti kwani maana kiisimu ni maana inayotokana na mfumo lugha na haiwezi kueleza maana ya msemaji. Kwa kutumia sitiari katika mawasiliano, maana inayofichika katika sitiari huhitaji kutafutwa kwa sababu maana inayopatikana-katika sitiari-inaweza kuwa inabeba mambo mbalimbali kuhusu jamii kama vile falsafa ya jamii kuhusu maisha.

#### 3.5.1 Sitiari dhanifu zenye leksimu moja

Sitiari dhanifu hukuza uwezo wa kuwasiliana na kuwaza. Sitiari hizi huweka wazi dhana fulani kupitia kwa dhana nyingine. Wakieleza sitiari dhanifu yenye leksimu moja, Ungerer na Schimid (2001:118) walitoa mfano *muda ni pesa*. Walisema kuwa, wanaisimu hufikiria sana kuhusu DL (*muda)* kupitia kwa *DC* (*Pesa)*. Hivyo sifa za *MUDA** zinatafutwa kutoka kwa *PESA**. Data msingi kuhusu “pesa” ni kuwa

a) Pesa ni kitu cha thamani
b) Ni raslimali haba.

Baadhi ya sitiari katika methali huwa ni sitiari dhanifu zilizo na leksimu moja. Sifa za sitiari hutusaidia kuunganisha fahiwa za leksimu katika kitengo kimoja na kuzihusisha na fahiwa za neno katika kitengo kingine. Hivyo, sitiari ya aina hii hutusaidia kutumia tajriba yetu kuelewa dhana/istlahi moja kwa msingi ya dhana/istilahi nyingine, hivyo hutusaidia kutumia uwezo wetu wa kiakili kuhusisha tunayojua na yale tusiojua. Mfano zaidi ya methali za sitiari zilizo za neno moja kama vile:

a) Ubishi ni ghasia
b) Utajiri ni umande
c) Akili ni mali.

#### 3.5.1.1 Sitiari zinazorejelea vitu vya kudhanifu

Vitu dhania, ni vitu ya kufikirika katika ulimwengu halisi au ni vifaa vilivyo katika ulimwengu wa kiudhanifu. Maneno ya aina hii yanapatikana katika mawasiliano kama sitiari katika lugha ya Kiswahili na lugha zinginezo. Sifa za vifaa dhania zinaweza zikahusiana na sifa za dhana nyingine kama vile au vifaa halisi au vifaa dhania. Baadhi ya sitiari dhania ni kama vile mapenzi, usemi, wazo na ujinga. Aidha aina za sitiari kama hizi zinapatikana katika methali ila hazionekani kubadilisha maana yake halisi kwa kiwango kikubwa.

**Mfano 1***:*

***Sumu ya neno ni neno***

Methali kama hii inaonekana kuwa inalinganisha dhana dhahania na dhana dhahania nyingine. SUMU YA NENO* inalinganishwa na NENO*. Methali yenyewe inatumiwa kuonyesha kuwa dawa ya neno kali ni kujibu neno hilo kwa neno lenye uzito sawa na hilo. Ufasiri wa sitiari hii unahitaji msikilizaji awezeshe DC yaani "*NENO"* ili kupata chukulizi za neno hili ambazo zitamwelekeza katika kupata fasiri za neno NENO. Ili kupata maana ya usemi huu, mfasiri atapanua dhana ya neno "*NENO"* kwa kuhusisha dhana maalum ya kihali ya NENO, ambayo huipa fasiri dhana ya sitiari kwa kulihusisha na muktadha itakayotumiwa ambao ni "sumu ya neno". Dhana ya "" itazuka na chukulizi zifuatazo katika vitomeo vya kienisaiklopedia:

a) Mkusanyiko wa sauti zinazotamkwa au kuandikwa.
b) Sauti zinazoleta maana
c) Jambo la maana
d) Jambo kubwa
e) Mahubiri
f) Neno kali



Alama ya Kinyota (*) inaashiria maana ya kisemantiki ya leksimu au kirai husika.

Kupitia kwa chukulizi hizi ambazo kwa hakika zinarejelea maana ya kimuktadha ya neno "*NENO"* na zinazopatikana katika enisaiklopedia, msikilizaji hufaa kufuata utaratibu fahamishi wa nadharia ya uhusiano ili kubaini namna *sumu ya neno* huwa *neno*. Kwa kufuata uhusiano baina ya sifa hizi, msikilizaji ataziteua sifa chache miongoni mwa sifa za jumla za dhana ya NENO ambazo zinaweza kurejelea SUMU YA NENO*. Ili kupata fasiri ya neno NENO msikilizaji atapaswa kuwezesha dhana ya NENO, achunguze seti za chukulizi zinazohusiana na dhana ya neno kuwa sumu kutoka ile ya mwanzo hadi ya mwisho, yaani (a-f), halafu ateue moja kati ya seti hizo ambayo itakuwa na uhusiano wa juu zaidi. Katika mkutadha huu, NENO* litapata maana mpya ya NENO KALI. Hii ni kwa sababu maneno yaliyotangulia kama vile SUMU YA NENO* yanaelekeza kuwa SUMU* inaua na ni hatari. Chukulizi (a-e) zitaachwa na (f) itachukiliwa kwa msingi ya kanuni tambuzi kwa sababu ndio chukulizi iliyo na uhusiano wa hali ya juu. Kwa kuchunguza muktadha wa matumizi, methali hii inamhimiza na kumkumbusha msikilizaji kuwa tayari kumkabili msemaji kwa neno sawa na lile atakalolitumia.

**Mfano 2**

***Dunia ni mapishano***

Dhana ya mapishano, kwa kawaida inamaanisha kuwekeana nafasi ili mtu fulani apitie. Uwezo wa DUNIA* kupisha kitu au mtu haupo. Dunia si binadamu hivyo, lazima msikilizaji au msomi atatakiwa kutumia dhana maalum ya kihali ili aweze kupanua neno MAPISHANO* hadi liafikiane na uwezo huu wa kupisha. Sifa maalum ya kihali itamsaidia kupanua maana ya neno MAPISHANO na kuibuka na chukulizi mbalimbali za neno hilo katika mchakato wa kutafuta maana. Uhusishaji wa dhana maalum ya kihali utasaidia kuzua chukulizi zifuatazo za dhana ya MAPISHNANO kwa msingi ya ensaiklopedia:

a) Weka nafasi ili mtu apite
b) Hali ya kupeana nafasi
c) Kutoa zamu kwa mtu mwingine
d) Kubadilishana nafasi, nyenzo hali baina ya watu wawili
e) Kutobaguana/ kuwekea nafasi sawa.
f) Kutochagua au kutotenga watu kwa msingi yoyote

Kwa kutuma kanuni za kiutambuzi msikilizaji huweza kuchuja chukulizi ambazo hazisaidii katika kupata uhusiano. Hivyo, chukulizi (a,b na c) zitafungiwa nje, na (d,e na f) ndizo zinazoleta uhusiano zaidi hivyo zinachukuliwa kwa kuwa na ufaafu wa juu katika kuleta maana ya kauli DUNIA NI MAPISHANO, Hivyo kauli hii itachukuliwa kumaanisha kuwa **duniani** kuna kubadilishana nafasi au kuna nafasi sawa duniani kwa wanaoishi humo. Hivyo, katika muktadha huu, methali hii inatumika kummotisha msikilizaji kwa kumhimiza kujaribu analonuia kulifanya maishani.

**Mfano 3**.

***Ahadi ni deni***

Kwa msingi ya nadharia ya uhusiano, msemaji anaposema kuwa AHADI ni DENI kauli yake itachukuliwa kuwa na thamani ya kumfanya msikilizaji kuichakata. Hivyo, atahitajika kufanya upanuzi wa neno DENI* ili kupata maana ya msemaji kwa sababu maana halisi ya neno ***deni*** humaanisha dai au kitu anachodaiwa mtu. Katika muktadha huu AHADI* haiwezi kudaika si DENI* hivyo maana halisi haitakidhi matarajio ya msemaji. Ili kutafuta maana ya msemaji, dhana maalum ya kihali itatumika ili kuleta upanuzi utakaosaidia kuleta maana ya msemaji. Kwa kutumia dhana maalum ya kihali, neno DENI hupanuliwa ili kukuza chukulizi mbalimbali za neno kulingana na kimuktadha, kanuni ya mawasiliano na kauli za msemaji. Vitomeo vya kienisaiklopedia kuhusu DENI vitakuza chukulizi zifuatazo.

a) Kitu anachodaiwa mtu
b) Kifaa chenyewe kinachodaiwa
c) Kitu kinachofaa kulipwa au kurejeshewa mwenyewe
d) Timizo la kiwango fulani.

Ili kufasiri kauli hii, nadharia ya uhusiano hutoa utaratibu fahamishi wa kiurejelezi ambao hufuatwa ili kupata fasiri ya tamko. Mchakato wa kufasiri huongozwa na chukulizi maalumu kuhusu uhusiano unaokubalika na wahusika wote (msikilizaji na msemaji). Kwa kutumia kanuni

za kiutambuzi, tutaweza kuchuja chukulizi ambazo hazisaidii katika kupata maana iliyo na uhusiano. Hivyo chukulizi kama (a-c) zitafungiwa nje kwa kuwa hazina uhusiano wa hali ya juu. Kisha, chukulizi (d) itachukuliwa kwani ndio iliyo na uhusiano unaochangia kuleta maana ya msemaji. Hivyo, ahadi inafaa kutimizwa. Methali hii inatumika kuwashauri na kuwakumbusha watu kutimiza ahadi zao. Aidha, methali hii itakuwa ikimsuta mtu ambaye anaahidi kitu na kukosa kutimiza.

**Mfano wa 4**

***Fedha ni fedheha***

Methali hii inapotumiwa kama kauli ya msemaji itaonekana kama kinaya inapochunguzwa maana ya juujuu na msikilizaji, ambaye huenda anaona fedha kama kitu cha kumletea raha. Wilson na Sperber, (2004) walieleza kuwa kuna utaratibu fahamishi wa kiurejelezi ambao msikilizaji atafasiri methali hii ambao hufuata mkondo huu: kwanza, kuchukulia kuwa msemaji amesema jambo linalochukuliwa kuwa linakuza matarajio fulani kama vile kufanya kitendo cha kujibu au kushauri msikilizaji. Pili, msikilizaji huanza kutafuta maana ya kilichosemwa yaani namna FEDHA* huwa FEDHEHA*.  Katika muktadha huu neno *fedheha* ndilo limebeba maana na ndilo linafaa kuchunguzwa. Ili kupata maana ya msemaji, msikilizaji atapaswa kuhusisha dhana maalum ya kihali na kuipanua maana ya neno FEDHEHA* kulingana na muktadha wa matumizi na maana aliyoikusudia msemaji. Dhana hii itazuka na chukulizi zifuatazo za neno ya FEDHEHA kwa misingi ya ensaiklopedia*:*

a) Jambo la aibu
b) Kitendo kinacholeta aibu
c) Hufanya  mtu kuona haja na kujitenga na wengine
d) Hufanya mtu kuchukiwa na wengine.
e) Hutenganisha watu

Tamko linalohusisha methali hii litaafikia uhusiano ikiwa litaangaliwa katika muktadha ambapo neno “fedheha” limetumika. Kwa hivyo msikilizaji atatumia kanuni tambuzi za uhusiano kupata chukulizi zilizo na maana kwa usemi ili kumwelewa. Hivyo, kwa msingi ya utaratibu fahamishi

atachukua chukulizi (d-e) na kuacha chukulizi (a-c). Methali hii itapochunguzwa katika matumizi yake basi itakuwa ikipinga fikira kwamba fedha zinaleta raha vilevile kumshauri kuwa fedha zinaweza kuleta aibu.

#### 3.5.1.2 Methali zinazotaja vifaa halisi

**Mfano 5**

***Mke ni nguo, mgomba ni kupalilia***

Nadharia ya uhusiano inadai kuwa maandishi/ tamko kama hili haliwezi kuchukuliwa ovyo, kwani, kanuni ya mawasiliano inatetea kuwa kila lisemwalo lina thamani ya kupitisha ujumbe. Mtu anaposoma au kusema ujumbe huu kwenye jarida au kwa leso ya mwenziwe ataupata ujumbe fulani ulionuia kupitishwa kwake kupitia kwa maandishi au tamko “MKE NI NGUO”*. Kwa kuwa MKE* hawezi kuwa NGUO* katika hali halisi, kauli hii itakuza matarajio fulani kwa msomaji. Hivyo, itambidi apanue maana ya neno NGUO kupitia kwa dhana maalum ya kihali. Kwa msingi ya upanuzi huo data za ensaikilopedia zitakuza chukulizi zifuatazo za dhana ya NGUO:

a) Vazi linalovaliwa ili kusitiri uchi
b) kitambaa chochote
c) vazi la kukinga mtu jua au baridi
d) Vazi linalomfanya mtu kuonekana maridadi na kupendeza
e) Ishara ya malezi mema
f) Utunzaji wa mlezi.

Wilson na Sperber (2004) waliteteta kuwa mchakato wa kufasiri matini hii utahusisha uchunguzi wa chukulizi zilizokuzwa kupitia dhana maalum ya kihali. Hivyo maana ya matini au tamko hili itakuzwa kuanzia msingi wa upanuzi wa maana leksika ya neno NGUO hadi kwa maana zinazokuzwa na muktadha ambao neno hili linatokea. Mfasiri atapaswa kutumia kanuni tambuzi za uhusiano ili kupata chukulizi zilizo na maana kwa ujumbe anaonuia kuupitisha msemaji/ mwandishi kupitia kwa leso au tamko. Uchaguzi wa chukulizi zilizo na maana utafanyika kwa msingi wa utaratibu fahamishi wa nadharia ya uhusiano. Hivyo, Chukulizi (a-d) ambazo hazileti

maana iliyo na uhusiano wa hali ya juu zitaachwa. Msikilizaji atapaswa kuchukua chukulizi (e na f) kwa sababu ndizo zilizo na uhusiano wa hali ya juu kwa kauli au matini hii. Dhana ya utunzaji inasababishwa na hali ya kupalilia mgomba. Tendo la kupalilia mgomba linakuza sifa ya utunzaji wa mti, hivyo, mke anapotunzwa, anaweza kutunzwa kwa namna nyingi ukiwemo wa kimavazi kama vile kununuliwa nguo. Methali hii inatumiwa kumshauri msikilizaji kutunza mke na kumkumbusha asiyetunza mkewe kuwa hakuna mke asiyependeza ikiwa atatunza na mmewe.

**Mfano 6**

***Upishi ni kuni***

Kauli kama hii ambayo inaweza kutolewa na mtu yeyote katika mawasiliano inaweza kukuza athari za kiutambuzi. Hivyo, inafaa kuchakatwa ili kupata maana ya msemaji. Maana ya methali hii kwa msingi wa muktadha halisi ilimotumika, inaweza kuwa katika vyote yaani kiwango cha juujuu au kiwango cha ndani. Inapotumiwa au kuambiwa mtu katika muktadha wa mapishi, basi, anayeambiwa uipata maana ya ujumbe unaowasilishwa katika maana ya kijuujuu. Lakini ikiwa imetumika katika muktadha tofauti na ule wa mapishi basi itamlazimisha msikilizaji kufiria kwa undani kwa sababu kuna maana nyingine iliyojificha katika kauli hii. Maana hii itabidi uchunguzi wa kina hufanywe kuhusu neno KUNI* kuipata maana ya ndani ya kauli UPISHI NI KUNI*, Ili kupata maana hii msikilizaji atahusisisha dhana maalum ya kihali ili kupanua maana ya neno KUNI kwa msingi ya enisaiklopedia, hivyo, ataweza kuzua data zifuatazo za dhana ya KUNI.

a) Kipande cha mti
b) Kilichokatwa au kuvunjwa kutoka kwa sehemu kuu ya mti
c) Kinakokea moto
d) Hutumiwa kuhifadhi moto
e) Vifaa vya kazi ni muhimu katika kazi hiyo (upishi).

Ili kufasiri tamko, msikilizaji atapaswa kuchunguza kauli/ neno KUNI katika kauli nzima ya UPISHI NI KUNI* katika muktadha wa kimatumizi. Methali hii hutolewa kama kauli ya kushauri msikilizaji. Hii ni kwa sababu uhusiano uliopo baina ya dhana ya “kuni” na ile ya

“upishi” ni ya kufaana Ufasiri huu utapatikana baada ya msikilizaji kutumia kanuni tambuzi za uhusiano kupata chukulizi zilizo na maana kwa usemi husika. Hivyo, atachukua chukulizi (f) na kuacha chukulizi (a-e). Maana maalumu ya kihali itakayopatikana ni kuwa; kazi hufaulu ikiwa vifaa vyote vya kazi hiyo vipo.

**Mfano 7**

***Pili pili ni mchanga***

Maana ya methali hii imo katika fasiri ya dhana ya neno MCHANGA. Nadharia ya uhusiano inadai kuwa ufahamu wa leksimu iliyotumiwa kisitiari katika methali huhitaji uundaji wa dhana maalum ya kihali ili kuafikia maana iliyokusudiwa ambayo inaweza kuafikiwa kupitia ama ubanaji au upanuaji wa maana leksika. Katika methali PILIPILI NI MCHANGA, Neno *mchanga* ndilo linalobeba maana kuu, kwa sababu ndilo linalofafanua neno PILIPILI*. Msikilizaji atapaswa kushughulikia dhana hiyo ili aweze kupata chukulizi zinazofaa na ambazo zinaweza kutoa maana inayokusudiwa na mtumiaji wa methali husika. Dhana ya “MCHANGA” itazuka na chukulizi zifuatazo katika vitomeo vya kienisaiklopedia

a) Chembechembe ya mawe yaliyopondeka au kusagika
b) Upandwa kitu kikamea
c) Ni sehemu inayodumisha maisha ya mbegu
d) Ni malezi unaompa mtoto/kitu kichanga.

Data hizi zote hurejelea MCHANGA* kwa jumla na huwa zimewekwa akilini ya msemaji au msikilizaji. Hata hivyo, ni data chache sana ambazo zinaweza kuchaguliwa ili kurejelea kifaa/ dhana inayofanana na MCHANGA. Hivyo msikilizaji atachagua sifa zinazofaa muktadha wa tamko na ataweza kuipata sifa moja ya pilipili ni kuwa kali na ukali wake hutokana na mahali ilipopandwa na kukulia. Lakini msikilizaji anapochunguza muktadha wa moja kwa moja ambapo neno **mchanga** limetumika, pamoja na maneno yaliyotangulia kauli hii, upanuzi zaidi wa dhana mchanga utahitajika. Hivyo, dhana maalum ya kihali ya MCHANGA hufanywa na data zifuatazo za kiensaiklopedia hupatikana. Ili data hii ipatikane, msikilizaji anaweza kuhitimisha kuwa dhana maalum ya kihali ya MCHANGA ni malezi. Hiyo methali ikaashiria kuwa kinacholelewa

hukua kama kinavyotunzwa na walezi wake. Katika muktadha huu methali hii inatumika kushauri wazazi dhidi ya kuwa mfano mbaya kwa wanao, kwani huenda wakaiga na kufuata mifano hii siku za baadaye. Kwa msingi hii msikilizaji ataelewa kuwa anashauriwa kuwa mtoto anafaa atunzwe vizuri ili aweze kukaa kama wanavyomtatajia wazazi wake.

**Mfano 8**

***Mtoto wa nyoka ni nyoka***

Katika mfano huu neno “nyoka” limetumika kisitiari kwa sababu neno hili linatumika katika muktadha unaomrejelea sifa za kiumbe NYOKA*. Leksimu hii inaweza kuwa na fasiri pana ambayo inaweza kuafikiwa kupitia urejelezi wa dhana iliyosimbwa. Urejelezi huu huhitaji ufahamu wa leksimu iliyotumika kisitiari katika methali. Hata hivyo, muktadha inamotokea leksimu fulani katika sentensi au methali huenda ikahitaji uundaji wa dhana maalum ya kihali ili kuafikia maana iliyokusudiwa ambayo inaweza kuafikiwa kupitia ama ubanaji au upanuaji wa maana leksimu hiyo. Methali MTOTO WA NYOKA* KUWA NYOKA*, maana ya juu ya methali yenyewe ni ya kweli kwa sababu haitarajiwi NYOKA* kumzaa mtoto asiyekuwa mwananyoka. Hata hivyo ikitumiwa kumrejelea mtu na uzao wake. Basi, itahitaji uwezeshaji wa dhana maalum ya kihali ili kupanua maana halisi ya neno NYOKA. Katika hali hii, msikilizaji atapata vitomeo vya kiensaiklopedia vifuatayo ya NYOKA:

a) Ni mnyama mrefu na mwembamba
b) Mwenye magamba na asiye na miguu
c) Hutambaa na hutaga mayai
d) Baadhi wana sumu na hula ndege, vijinyama vidogodogo kwa kuvimeza
e) Huuma
f) Udhaniwa kuwa mjanja

Data hizi zote hurejelea mnyama aina ya NYOKA kwa jumla na huwa zimewekwa akilini ya msemaji au msikilizaji. Kanuni ya utambuzi humsaidia msemaji au msikilizaji kuchagua data chache miongoni mwa data nyingi ili kurejelea kifaa/dhana inayofanana na NYOKA. Hivyo msikilizaji atachagua sifa zinazofaa muktadha wa tamko na ataweza kujua kuwa NYOKA* huweza kuuma ana ujanja au humeza vinyama vidogovidogo. Lakini msikilizaji anapochunguza

muktadha wa moja kwa moja ambapo sitiari hii imetumika pamoja na maneno yaliyotangulia kauli hii atapanua maana ya dhana NYOKA zaidi hivyo anaweza kuibuka na maana ya mzazi asiye na tabia au maadili mema. Hivyo, dhana maalum ya kihali ya humwezesha msikilizaji kuhitimisha kuwa dhana maalum ya kihali ya NYOKA ni tabia au sifa fulani za mzazi. Hiyo methali ikaashiria kuwa mtoto hafunzwi tabia za wazazi wake bali huzipokea barabara kutoka kwa wazazi wake. Msikilizaji aidha, atagundua kuwa anakumbusha kuwa tabia za mzazi huenda zikarithiwa na mtoto. Kutokana na muktadha ambamo methali hii imetumika, msikilizaji ataelewa kuwa anashauriwa kuwa mtoto anafaa atunzwe vizuri ili aweze kukaa kama wanavyomtatajia wazazi wake.

### 3.5.2 Mawasiliano kupitia kwa sitiari zenye muundo wa kirai

**Mfano** 9.

***Mgeni ni kuku mweupe***

Kulingana na kanuni ya mawasiliano katika nadharia ya uhusiano, msikilizaji hustahili kusaka maana katika mawasiliano yoyote mpaka aipate maana anayoitarajia kuwa na uhusiano wa juu kwa usemi husika. Katika diskosi hii, mtu anaposema kuwa "mgeni ni kuku mweupe", inakuwa dhahiri kuwa analinganisha dhana moja na dhana nyingine kwa njia ya moja kwa moja. MGENI* inalinganishwa na KUKU MWEUPE*. Maana halisi ya neno "**KUKU***" na "**MWEUPE***" ni maana katika umbo la kimantiki. Katika muktadha huu, neno "**kuku mweupe**" limemiliki sifa fulani na limetumiwa kisitiari kumrejea **MGENI*,** (ambaye pia ana sifa zake). Nadharia ya uhusiano hudai kuwa mtu anaposema au kuandika usemi kama huu, itachukuliwa kuwa msemaji ametamka kauli iliyo na maana ambayo msikilizaji anafaa kuisimbua. Kwa kuwa "*mgeni*" hawezi kuwa "*kuku mweupe*" katika hali halisi, msikilizaji atalazimishwa kutumia dhana maalum ya kihali na kupanua maana ya kirai "*kuku mweupe*" kwa kukihusisha na muktadha, data za kienisaiklopedia na kanuni za mawasiliano. Hii ni kwa sababu usemi huu haufikii kiwango cha matarajio ya uhusiano. Kwa kutumia dhana maalum ya kihali na kanuni ya mawasiliano, msikilizaji hupaswa kutajirisha kirai "*kuku mweupe*" kwa kutumia dhana hii. Chukulizi mbalimbali zitakuzwa kwa kuzingatia muktadha wa kimatumizi wa neno KUKU MWEUPE* ili kupata maana ya msemaji. Hivyo, data ya kienisaiklopedia itakayopatikana ya neno *kuku mweupe* itakuwa:

a) Ndege anayefugwa nyumbani anayefanana na kware
b) Kuku mwenye manyoya meupe
c) Kuku asiyeweza kufichika kwa kutokana na rangi yake
d) Kitu kinachoonekana kwa haraka
e) Kitu/mtu anayetambulikana haraka.

Sifa ya kiisimu ya neno "KUKU MWEUPE*" haiwezi kuridhisha matarajio ya uhusiano kwa sababu itatupatia maana ambayo ni tofauti kidogo na maana ya msemaji, kwa hivyo, msikilizaji anafaa kutafuta maana iliyo kati ya maana kiisimu na maana ya msemaji. Hivyo, ujuzi wa kienisaiklopedia pamoja na ule wa kimuktadha ambao kauli hii imetumika, utatumika katika mchakato wa kutafuta maana. Baadaye chukulizi nyingi kutoka kwa ulimwengu zitachunguzwa ili kupata namna "*MGENI**" huweza "*KUKU MWEUPE**". Kwa kufuata njia yenye ufinyu, msikilizaji ataanza kuchunguza chukulizi hizi kwa misingi ya utaratibu fahamishi wa nadharia ya uhusiano. Baada ya hayo, msikilizaji atahusisha kanuni tambuzi "kuzichota" sifa ambazo zina uhusiano wa hali ya juu na kauli hii kwa msingi ya urejelezi. Hivyo, ataweza kuelewa kuwa

*mgeni* huonekana na hutambulika haraka. Mchakataji atafungia nje chukulizi (a),( b) na (c) kuchukua (d na (e) ambazo ndizo zilizo na uhusiano wa juu zaidi na maana ya msemaji. Pamoja na hayo, msikilizaji atagundua kuwa methali hii inamshauri kuwa ni rahisi kumtambua mtu ambaye anakusudia kufanya jambo fulani kutokana na tabia au mavazi aliojivalia.

**Mfano 10**

***Maneno ni jangwa tembezi***

Methali hii inatumiwa kuonyesha hali halisi ya maneno na kuwatahadharisha watu dhidi ya kunenanena kuhusu mambo ya watu ovyoovyo. Maana ya juujuu ya kauli hii, inakuza fenomena inayoitwa uhishi wa kisitiari au prosopopeia ambapo kitu hupewa sifa maalumu kutoka kwa mtu au wanyama. Hii ni kwa sababu kiashiriwa JANGWA* hakiwezi kutembea katika hali halisi aidha MANENO* hayawezi kuwa JANGWA* inayotembea. Lakini kwa msingi wa nadharia ya uhusiano, msikilizaji anafaa kuchukulia kuwa msemaji amesema kitu kilicho na ujumbe unaohitaji kusimbuliwa. Ujuzi huu utamsaidia yeye kukuza matarajio ya kile msemaji alinuia kusema ndipo ajenge chukulizi chake kuhusu kauli yake.

Kwa kuwa maana kiisimu, hairidhishi matarajio ya uhusiano, msikilizaji atatakiwa kutafuta maana iliyo kati ya maana kiisimu na maana ya msemaji. Hivyo, kutakuwa na uhusishaji wa dhana maalum ya kihali na kanuni za mawasiliano. Upanuzi utakaopatikana utazua sifa zifuatzo za ensaiklopedia za dhana *JANGWA* TEMBEZI**

a) Eneo kame lisilo na maji
b) Eneo lisilo na watu
c) Mahali hatari kwa wanyama na watu
d) Jambo hatari linaloenea haraka kila wakati
e) Jambo linaloenea na kuwasumbua watu.

Baada ya kuorodhesha sifa hizi, msikilizaji huhitaji kutumia kanuni za kiutambuzi kuteua pembejeo zilizo na uhusiano unaofaa kutoka kwa orodha ya chukulizi zilizokuzwa, kwa msingi ya mfumo wa kiurejelezi. Msikilizaji atazichakata pembejeo hizi kwa njia iliyo bora ya uzalishaji kwa msingi ya utaratibu fahamishi wa nadharia ya uhusiano. Baadaye "atachota" sifa zilizo na uhusiano wa juu zaidi ya kauli husika kutoka kwa chukulizi alizounda. Kwa kufuata njia yenye ufinyu wa kiuwezo katika kupata athari za kiutambuzi, msikilizaji ataacha chukulizi (a), (b)

na(c) na kuchukua chukulizi (d) na (e) kwa sababu ndizo zilizo na uhusiano wa hali ya juu. Hivyo, ataelewa kuwa maneno mabaya ni hatari na yanaweza kusambaa kwa kila insi na kuwaudhi wanaorejelewa au kuleta maangamizi na masumbuko kwa wanajamii. Methali hii ikichunguzwa kulingana na muktadha wa matumizi itaonekana kuwa babu anapitisha ujumbe unamuonya mjukuu dhidi ya kuzungumza maneno ya watu ovyoovyo haswa mambo yasiyofaa, huku, ukimlaumu anayezungumziwa kwa kuwa mdaku na mwenye kuzungumza mambo ya watu na ovyo ovyo kwa kila mtu/watu bila kujali madhara yake.

**Mfano 11:**

***Maisha ni mshumaa uso mkesha***

Ulinganishi wa aina hii ni wa kisitiari. Unalinganisho wa MAISHA* na MSHUMAA* unahusisha fenomena ya sitiari inayojulikana kama ufumbaji wa kimaongezi ambapo dhana hubandikwa jina la dhana nyingine kwa msingi ya kufanana kwa sifa fulani. Kauli kama hii inaposemwa na kasisi kwa waumini haitaeleweka kwa urahisi ikiwa maana yake itaangaliwa kijuujuu. Kwa hivyo, kauli hii itafaa kuchunguzwa kwa ndani ili kupata maana yake. Nadharia ya uhusiano inadai kuwa kauli ya msemaji inafaa kuchukuliwa kuwa na thamani inayomstahili msomaji/ msikilizaji kuichakata. Hivyo, msikilizaji anapoisikia kauli hii ataichukulia kuwa na thamani hii. Atapaswa kuchunguza Kirai MSHUMAA USO MKESHA* ili kupata maana ya maisha kutokana na kirai chenyewe. Atakitajirisha kirai hiki kwa msingi ya muktadha ili kukuza chukulizi mbalimbali. Sifa za kiensaiklopedia za “mshumaa uso mkesha” zitakuwa kama ifuatavyo:

a) Mche duara unaotengenezwa na nta
b) Unagandanishwa kwenye utambi wa taa
c) Hutumiwa kumlikia usiku
d) Huyeyuka unapochomwa ili kutoa mwangaza
e) Haidumu ukiangaza,
f) Huisha.

Kwa kuwa sifa za kiisimu za dhana hizi mbili haziridhishi matarajio ya uhusiano, Msikilizaji atahitajika kutafuta maana kati ya maana kiisimu na maana ya msemaji. Kwa kutumia ujuzi wa

kimuktadha na wa kienisaiklopedia ambao kauli hii imetumika, pamoja na kuhusisha chukulizi walizonazo za kilimwengu, waumini wataweza "kuchota" sifa zilizo na uhusiano zaidi katika kauli hii kwa msingi ya kanuni tambuzi. Chukulizi zilizo na uhusiano wa hali ya juu na kauli ya kasisi zitafikiwa kwa msingi ya utaratibu fahamishi. Wakati uhusiano huu utakapopatikana ndio uchakataji na ufasiriaji wa maana utakoma. Hivyo, msikilizaji atachukua chukulizi (e) na (f) na kuacha chukulizi zisizofaa. Hivyo, dhana maalum ya kihali ya kirai MSHUMAA USO MKESHA itakuwa kitu kisicho na uwezo wa kudumu. Sifa hii inatokana na uwezo wa mshumaa kukosa kudumu usiku kucha ukiwaka. Muktadha ambao methali hii imetumika, hunaonyesha kuwa methali hii inatumiwa kuwakumbusha Wakristo kuwa maisha hayadumu hivyo inawashauri kujipanga kwa maisha ya baadaye.

***Mfano 12***

***Ujirani ni fedha katika kasha***

Ikiwa methali hii imetamkwa na jirani A akimzungumzia Jirani B. itambidi Jirani B kuchunguza usemi huu ili kupata maana ya jirani mwenzake. Kwa kuwa ujirani huwezi kuwa FEDHA* iliyowekwa kwenye kasha, msikilizaji atapaswa kutumia dhana maalum ya kihali ili kupanua maana ya neno "FEDHA KATIKA KASHA*. Data za ensaiklopedia za FEDHA KATIKA KASHA itakuwa:

a) Pesa zilizowekwa kwenye sanduku kubwa la chuma
b) Pesa katika sanduku ngumu
c) Pesa zilizowekwa mahali salama
d) Kitu cha thamani kinachofaa kutunzwa vizuri.
e) Kitu cha kumfaa mtu leo na siku za usoni.

Kwa msingi ya nadharia ya uhusiano, msikilizaji atatumia kanuni za utambuzi na kuchagua chukulizi zilizo na uhusiano zaidi kuhusu kile alichonuia kukisema msemaji kwa kusema kuwa JIRANI NI PESA KATIKA KASHA. Jirani B hustahili kuchunguza chukulizi hizi hadi aipate maana ya Jirani A kulingana na muktadha pamoja na kanuni za mawasiliano. Dhana maalum ya kihali ya FEDHA KATIKA KASHA ni kuwa ujirani una thamani na umuhimu kwa wanajamii

siku za leo na baadaye. Hivyo, atachagua chukulizi (d) na (e) na kuacha (a-c) ambazo hazina uhusiano wa juu zaidi.

**3.6 Hitimisho**

Matokeo katika sura hii yamedhibitisha kuwa maana za methali za sitiari dhanifu huwa katika viwango viwili; kiwango cha juujuu na kiwango cha ndani. Kiwango cha juujuu hupatikana

katika maana ya juu na kiwango cha ndani hupatikana katika maana ya ndani ya methali. Hata hivyo, maana ya neno hutokea katika muktadha na hufasiriwa kulingana na muktadha ambamo methali husika hutumika.

Aidha, kwa kuchunguza maana ya juu juu ya dhana au istilahi zilizotumika au kulinganishwa katika methali, tutaona kuwa, kuna ulinganifu unaozua uhusiano ama kwa njia bayana/bainifu au pengine kwa njia isiyo bayana baina ya dhana hizo. Kwa mfano, baadhi ya ishara zinaweka wazi uhusiano baina ya ishara, hivi kwamba, ishara katika upande wa kwanza inalingana na kuhusiana na ishara ya pili katika mazingira halisi ya kimatumizi. Hivyo, maana ya methali kama hizi ni bainifu na inaeleweka moja kwa moja, hasa maana ya juujuu ikiangaliwa. Hali hii ni tofauti na methali ambazo hulinganisha ishara zilizo na uhusiano wa mbali kwa mfano: *Ujana ni tembo la mnazi, halikawii kupita, Sheria ni msumeno, hukata mbele na nyuma, Umaskini ni ngozi,* na *Kichwa ni shajara*

Katika kufasiri sitiari, muktadha ni muhimu na una mchango mkubwa wakati wa kufasiri maana ya neno lililotumika kisitiari ambapo maana ya neno msingi na ile ya neno la pili huathiriana katika harakati za kutafuta huhusiano uliopo baina ya dhana husika. Halkadhalika, muktadha linapotumika neno, unaweza kuathiri maana halisi ya neno husika na kulifanya kubadilisha maana yake ya kiisimu na kupata maana mpya. Huu ndio mchakato ambao sitiari zilizotumika katika methali hupitia ambao husababisha leksimu fulani kupata maana mpya.

Muktadha halisi linamotokea neno au methali nzima unaweza kudumisha au kubadilisha maana. Tumeona kuwa methali UPISHI NI KUNI inaweza kudumisha maana yake ikitumika katika muktadha wa upishi ambao labda mpishi amekosa kuni. Aidha MTOTO WA NYOKA NI NYOKA pia inadumisha maana yake katika muktadha halisi. Lakini sitiari hii au methali nzima ikitumika katika muktadha mwingine basi maana yake lazima ifasiriwe kwa kina kuambatana na muktadha huo**.** Aidha muktadha iiyozalika methali huchangia katika harakati za kutafuta maana ya methali husika kwani ujuzi wa muktadha huu huzua msingi wa kufasiri methali.

Kipragmatiki, leksimu inayorejelea dhana za kidhahania haibadiliki sana kimaana. Pengine, leksimu nyingine zinazorejelea dhana dhanifu, zinaweza kudumisha maana halisi au ikabadilika kidogo. Hivyo, maana ya maneno ya dhana hizi yanaweza kuhusiana au kukaribiana sana na maana halisi ya neno husika. Lakini maana halisi ya neno linalorejelea kifaa halisi, linapotumika

kisitiari linapoteza maana yake halisi na kuchukua maana iliyo kando sana na maana halisi ya neno husika. Mfano neno MCHANGA* kurejelea malezi au neno NGUO* kurejelea utunzaji.

# SURA YA NNE

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 4.1 Utangulizi

Utafiti wetu ulilenga kuchunguza namna leksimu au kirai hupata maana mpya katika methali za sitiari haswa methali ambazo hutambulisha kitu kimoja kwa msingi ya kitu kingine. Katika uchunganuzi wetu, mambo kadha kama vile: tamko, ujuzi wa ulimwengu wa kienisaiklopedia na muktadha wa matumizi huwa na mchango mkubwa katika ufasiri wa dhana. Utafiti wetu ulifanywa kwa msingi ya nadharia ya uhusiano na ulilenga kubainisha kama upanuzi na ubanaji wa maana ya neno unaweza kueleza kikamilifu neno lililotumika kisitiari na kuzua maana ya methali ya Kiswahili. Tumetathmini nadharia tete zetu ili kubainisha kama zinaunga mkono utafiti huu au zinapinga matokeo ya utafiti wetu.

## 4.2 Muhtasari wa matokeo ya utafiti

Matokeo ya utafiti huu yamebainisha yafuatayo. Kwanza, methali zote hutumika kama kauli katika mawasiliano au mazungumzo kwa lengo mbalimbali ikiwepo lengo la kushauri, kuelimisha, kuonya, au kuelekeza. Methali za sitiari dhanifu hufanya hivi kwa kutumia neno kisitiari ambapo neno hutambulishwa kwa neno lingine kwa kutumika katika muktadha fulani. Mabadiliko yanayokumba neno katika utambulisho huu yanaweza kuelezwa kupitia nadharia ya uhusiano. Jambo hili hutokea katika msingi ya upanuzi wa kidhana unaofanywa kwa misingi ya kuhusiana kwa sifa za dhana zinazolinganishwa. Upanuzi wa kisitiari unaleta maana kipragmatiki za leksimu iliyotumika katika muktadha.

Pili, utafiti huu umebainisha kuwa maana ya neno lililotumika kisitiari hutegemea muktadha wa matumizi. Maana ya kauli/ neno lililotumika kisitiari inaweza kubadilika au ikabaki namna iyo hiyo. Kwa mfano msemaji anaposema kwa msikilizaji methali “upishi ni kuni” katika muktadha wa mapishi, maana itapatikana moja kwa moja kutoka kwa kauli hii. Hata hivyo, maana inaweza kuwa tofauti ikiwa methali hii itatumiwa katika muktadha usio wa mapishi kama vile muktadha wa ujenzi.

Tatu, utafiti huu umebainisha kuwa methali hutumiwa kwa majukumu mbalimbali, yakiwemo kushauri, kuonya, kuelimisha, kutahadhari au kuelekeza msikilizaji, majukumu haya husababishwa na matumizi ya methali katika muktadha maalumu.

Nne, Utafiti wetu aidha umebainisha kuwa watumiaji wa sitiari wanafaa kuwa wanashiriki wa tamaduni moja Hivyo, msemaji wa sitiari na mfasiri wa sitiari hiyo wanapaswa kuelewa dhana iliyoyumika na falsafa zake. Hii ni kwa sababu methali za sitiari huundwa kutokana na kufanana kwa sifa moja au zaidi za dhana zinazolinganishwa ili kuunda methali za sitiari.

Tano, utafiti huu umebainisha kuwa, kunaweza kuzuka kutoelewana, ufasiri usiofaa na uvunjikaji wa mawasiliano haswa ikiwa neno litatumika kutambulisha neno lingine kwa sababu upanuzi wa sitiari huchochea kubadilika kwa maana. Upanuzi wa dhana ya kisitiari hutegemea sifa za dhana chanzi uinayolinganishwa na nyingine (Dhana lengwa) katika methali za sitiari. Hata hivyo, ni muhimu kutumia muktadha ambamo neno limetumika ili kuafikia maana sahihi ya kufasiri neno lililotumika kama sitiari.

## 4.3 Hitimisho

Matokeo ya utafiti huu yamehitimisha kuwa, mawasiliano kupitia methali za sitiari huhitaji wahusika kuwa na misingi sawa ya utamaduni kuhusu dhana husika. Ujuzi huu humfanya msemaji na msikilizaji kufanya urejelezi unaofaa wa ujumbe uliotumia methali za sitiari. Watu wanafahamu methali za Kiswahili vizuri wanafasiri leksimu ya Kiswahili kwa njia sahihi kupitia upanuzi au ubanaji ilhali wasiofahanu methali na dhana fulani za methali wanaweza kukosa kufahamu methali hizo/ hiyo. Nadharia ya uhusiano inadai kuwa kutokuwa na ujuzi kuhusu dhana zilizotumika katika sitiari kunaweza kusababisha kutofaulu kwa mawasiliano.

## 4.4 Mapendekezo

Utafiti huu ulilenga kuchunguza namna leksemu katika methali za Kiswahili hubadilisha maana yake halisi na kupata maana mpya. Utafiti wetu ulitathmini leksimu katika methali za kisitiari katika lugha ya Kiswahili kwa msingi ya nadharia ya uhusiano.

Utafiti huu unapendekeza kuwa, utafiti zaidi unaweza kufanywa kuhusu yafuatayo:

Kwanza, utafiti hufanywe kuhusu misingi ya kubainisha dhana tata ya sitiari ya Kiswahili ili kubainisha msingi dhabiti ya kufafanulia sitiari ya aina hii.

Pili, utafiti unaweza kufanywa kuhusu namna mikitadha mbalimbali kama vile miktadha ya kisaikolojia, kifalsafa na kijamii huweza kuzua methali hivyo kuchangia katika kupata maana ya sitiari husika.

Tatu, utafiti zaidi kuhusu methali za sitiari, hufanywe kwa msingi ya nadharia mbalimbali kama vile nadharia ya sitiari ya Lakoff na Johnson (1980) ili kutathmini maana ya  ziada ya sitiari za methali katika matumizi.

## MAREJELEO


Anyim, (2010) "Sense Relation in Dholuo". University of Nairobi, Tasnifu ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Nairobi

Assimakopoulos, S. (2008). *Logical Structure and Relevance.* University of Edinburgh.

Blass, (1990). "*Relevance Relation in a Discourse*. A Study with Special reference Sissala Cambridge". Cambridge Univeristy press.

Blutner, R. (1998) "Lexical Pragmatics in Journal of Semantics" Volume 15 (2) page 115-165.

Hock &Joseph, (1996), *Language Change, Language History, and Language Relationship and Introduction to Comparative Linguistics*. Newyork Mountain de Grugler

Horn, L. (2004)."Implicature". In Horn & Ward: 3-28.

Horn, L. & Ward, G. (eds.) *The Handbook of Pragmatics.* Oxford: Blackwell

Kobia, J.(2005)."Taswira ya Mwanamke katika Methali (Njuno)za kimeru" Tasnifu ambayo haijachapishwa. Moi University.

Kimani, (2004). "The Analysis of Truth Conditions in Pragmatics" :Relevance Theory Approach. Tasnifu ya MA University of Nairobi.(haijachapishwa)

Kingei K & Ndalu A, (2008) *Kamusi ya Methali* (Toleo jipya) EAEP Nairobi Kenya

Kinlon, (2005)."*Anthopology of Performance* katika Kihore", *Y.M.* (Mhariri) Kiswahili Juz 65. Tuki, Dar el Salaam

Levins, (1977).*The Semantics of Metaphor.* Maryland: The John Hopkins University press

Levinson, (1983).*Pragmatics.* London Cambridge University Press.

Mkota A, (2009) *Kamusi ya Methali Maana na matumizi,* Vide-muwa publishers Nairobi

Msokile, M. (1993).*Msingi ya Uhakiki wa Fasihi.* East Africa educational Publishers

Mutwiri, G. (2005).“Mtazamo kuhusu Utendakazi wa Nyimbo za Kiasili” Tasnifu ya M.A. Kenyatta University

Ndungu, C. (2006).”Matumizi ya Tamathali za Usemi katika Lugha ya Kisasa Katika Njogu K. Na Wengine (wahariri)” *Fasihi Simulizi ya Kiswahili* Twaweza communications, Nairobi uk 107-111.

Ndirangu, D.M. (2011). “*Kenyans Indeginous Redio Stations and their uses of Metaphor in 2007 Election Violence*”. Http/www / ingenitaconnect.com/ content / intelligent/jams;session.d=13b70ks5hp8ut.alice

Noordin, M. (2006).“Simulizi Maalum ya Pepo kama Ufasiri wa Fasihi Simulizi” . Katika Njogu K., Momanyi C. Na Mathooko M. *Fasihi Simulizi* Twaweza Communication na Chakita Nairobi

Nsookwa, C.J. (2011).*Dokezo za Sitiari katika Methali za Kiswahili na Kiluganda* “http//mak.ac.ug/doc

Nunberg, (2004).*The Pragmatics of Deffered Interpretation,In Horn and Ward (eds) The Handbook of Pragmatics U.K.*

Nyaga, D. (1986). “Mikarire na Miturire ya Ameru: Nteto cia Bajuju Betu:” Nairobi; EAEP. Publishers

Onish and Morphy, G. (1993). *Metaphoric Reference.* “When metaphors are not Understood as easily as Literal expression, Memory and cognition”. M.A Dissertation.

P’biket, O. (1973). *AfricaCulture Revolution;* Heinemann Educational Publishers Nairobi.

Richard R. (1995). *Semantics.* Newyork. Macgraw-Hill Book Company

Robert, B. (1970). *Semantic and Language Analysis*: New York Bobbs. Merill Company Library USA.

Shelestiuk H.V. (2003) *Semantic of Symbol* Semiotica 144(1/4), 233-259

Shelestiuk (2006), "Approach to Metaphor*: Structure, Classification, Cognate Phenomena in Metaphor"*. *Simiotica* 161-1/4 pg 333-343

Schroeder, H. (2005) "Do we Speak the Same Language?" A Cognitive Pragmatics, Explanations of Culture Misunderstanding in *Across the Border.* Benefiting from Cultural Differences. The paper originally presented at the international conferences on Africa, globalization and justice at the Catholic University Of East Africa, Center for Socio Justice and Ethics, NBI 17th -19th May 2006.

Soi (2014), "The Study of Selected Kipsigis Provebs, *A Case study in Kaplalech division."* Tasnifu ya MA: University of Nairobi.

Sito P.S. (2015) , "Athari za Mazingira katika Uteuzi wa Msamiati: Mfano methali za Kiswahili zinazorejelea viumbe wa majini. Tasnifu ambayo haijachapishwa Chuo Kikuu cha Nairobi

Sperber, D. & Wilson, D. (1995), *Relevance: Communication and Cognition*. Oxford: Blackwell.

Sperber D.& Wilson D, (2004). "*Relevance Theory in Horn and Wards (eds) The Book of Pragmatics".* United Kingdom Blackwell Publishers

Sperber, D. & Wilson, D. (2012).*Pragmatics*. In Wilson & Sperber 2012: 1-27.

Tarasova V.N. (1975) "On syncretism of metaphor: *In Expressive Means in the English Language"* 103-117 Leningrad: Progress.

Trudgil, P. (1995).Socio-linguistics: *An Introduction to Language and Society*. 3rd Edition. London, Penguin book.

Wacharos, J. (2013). "Kanga kama Sajili Maalum ya Kisanii na Mawasiliano" Tasnifu ya MA Chuo Kikuu cha Nairobi.

Wale (1989). *Dictionary of Stylistics.* London and Newyork.: Longmann.

Wamitila K. W. (2003).*Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi Focus Publication.

Wilson (2000). *Lecture notes on Issues of Pragmatics*. Lexical pragmatics PLIN 3001

Wilson & Cartson (2007)."*Unitary Approach to Pragmatics.* Relevance, Inference, and *Ad-hoc* Concepts in Nooel Burton (ed) Pragmatics" . London Palgrass

Wilson, D. & Sperber, D. (2004). *Relevance Theory.* In Horn & Ward: 607-632.

Wilson, D. & Sperber, D. (2012). *Meaning and Relevance.*Cambridge University Press.

## VIAMBATISHI

**SITIARI HURU**

1. Ajuaye ni mungu (Mkota,Uk. 16)
2. Akiba ni iliyo kibindoni (Mkota, 18
3. **Dunia ni mapishano (Kingei & Ndalu; methali 408)**
4. Elimu ni bahari (Kingei & Ndalu; methali 424)
5. Afya ni mali (Mkota,uk.11)
6. Elimu ni habari (Kingei & Ndalu; methali 425)
7. Fadhila ni utumwa (Kingei & Ndalu; methali 436)

   **Fedha ni fedheha (Kingei & Ndalu; methali 444)**
8. Imara ya chombo ni nanga (Kingei & Ndalu; methali 591)
9. Hata kiporo ni ugali (Kingei & Ndalu; methali 536)
10. **Ahadi ni deni (Kingei & Ndalu; methali 26)**
11. Asiyekosa ni malaika (Kingei & Ndalu; methali 158)
12. Akili ni mali (Kingei & Ndalu; methali 51)
13. Akili ni nywele (Kingei & Ndalu; methali 52)
14. Bahati ni chudi (Kingei & Ndalu; methali 229)
15. Asili ya mtu ni vumbi (Mkota, 46)
16. Asiyekosa ni malaika (Mkota,uk. 54)
17. Bahati ni upepo ( Kingei &Ndalu; 230)
18. Bandari ya maisha ni mauti (Mkotta uk.72)
19. Bei ni mghalaba (Mkota,uk. 74)
20. Biashara ni hesabu (Kingei & Ndalu; methali 251)
21. Bidii ni gongo (Mkota,uk.76)
22. Cheo ni dhamana (Kingei & Ndalu; methali 320)
23. Chembe na chembe ni mkate (Mkota,uk. 90)
24. Dalili ya mvua ni mawingu (Mkota,uk. 100)
25. Damu ni nzito kuliko maji (Kingei & Ndalu; methali 362)
26. Dhamira ni dira (Kingei na Ndalu 380)
27. Dhamira safi ni tandiko laini. (Kingei & Ndalu; methali 381)
28. Dunia ni maabara (Mkota,uk. 113)

29. Dunia ni darubini (Mkota,uk. 113)

30. Dunia ni watu (Mkota,uk. 112)

**31. Dunia ni mapishano (Mkota,uk. 112)**

32. Ivushayo ni mbovu (Kingei & Ndalu; methali 601)

33. Jirani ni ndugu (Kingei & Ndalu; methali 627)

34. Juhudi ni uokozi (Kingei & Ndalu; methali 645)

35. Kaa ni mfalume gandoni (Kingei & Ndalu; methali 652)

36. Kauli ni bora kuliko mali (Kingei & Ndalu; methali 678)

37. Kelele nyingi ni makeke (Kingei & Ndalu; methali 691)

38. Kutoa ni kujiwekea (Mkota,239)

39. Kichwa ni shajara (Kingei & Ndalu; methali 710)

40. Kusema ni fedha kujibu ni dhahabu ( Mkota,237)

41. Mauti ni faradhi (Mkota,uk. 282 )

42. Mchoo ni ukoo (Kingei & Ndalu; methali 1208)

43. Mtoto wa nyoka ni nyoka (Kingei na Ndalu methali; 1493)

44. Mzigo wa chungu, ni chembe moja ya mchele (Kingei & Ndalu; methali 1724)

45. Nguvu za mamba ni maji (Kingei na Ndali methali 1811)

46. Nyege ni kunyegezana (Kingei na Ndalu; methali,1847)

47. Penzi la moyo ni dawa (Kingei na Ndalu; methali, 1936)

48. Tabia ni ngozi ya mwili (Kingei & Ndalu; methali)

49. Umaskini ni ngozi (Kingei & Ndalu; methali 2249)

50. Upaji ni akiba (Kingei & Ndalu; methali 2277)

**51. Upishi ni kuni (Kingei & Ndalu; methali 2080)**

52. Utajiri ni msimu (Kingei & Ndalu; methali 2361)

53. Usiku ni libasi bora (Kingei & Ndalu; methali 2312)

54. Ukubwa ni jaa. (Kingei & Ndalu; methali 2227)

55. Safari ni hatua (Kingei na Ndalu; methali 1970)

56. Sahau ni dawa ya waja (Kingei & Ndalu; methali 1974)

57. Kuishi ni dhamiri (Mkota,uk. 224)

**58. Sumu ya neno ni neno (Kingei & Ndalu; methali 2064)**

59. Siasa si tanga ni nanga (Kingei & Ndalu; methali 2115)

60. Toba ni kitendo (Kingei & Ndalu; methali 2099)

61. Ugenini ni kweusi (Kingei & Ndalu; methali 2128)

**62. Pilipili ni mchanga (Kingei & Ndalu; methali 1940)**

63. Muungwana ni kitendo (Mkota,uk. 366

64. Mwanamme ni mbono hualika kule (Mkota,uk. 376

65. Mwanzo wa ngoma ni lele (Mkota,uk. 387

66. Kila mwanzo ni mzito ( Mkota,uk. 201)

67. Kiraka cha jamvi ni miyaa (Mkota, uk. *209*)

68. Ndovu akitamba ni masika (Mkota,uk. *404)*

69. Nguvu ni maarifa (Mkota,uk. *414*

70. Maisha ni jangwa tembezi (Kingei & Ndalu; methali 1108)

71. Njaa ni mwalimu (Mkota,uk. *418*

72. Nyumba ni mwanamke (Mkota,uk. *426*

73. Riziki ni kujaribu (Mkota,uk. 450

74. Salamu ni kikoa (Mkota,uk. *454*)

75. Sifa ya utungo ni mtindo (Mkota,uk. *462)*

76. Sifa ya nguo ni pindo (Mkota,uk. *462)*

77. Simba ni mrarua nyama (Mkota,uk. *466*)

78. Simba ni ngurumizi (Mkota,uk. *466*)

79. Starehe ni kivuli cha miba (Mkota,uk. *470*)

80. Tendo ovu ni kovu la milele (Mkota,uk. 476

81. Tikiti ni moto wa kwanza (Mkota,uk. 478)

82. Tui ni lile la kwanza (Mkota,uk. *480)*

83. Mlafi ni mtumwa wa mali (Mkota,uk. *324)*

84. Mila za biladi ni sheria (Mkota,uk. *308)*

85. Moyo wa mtu ni chuo (Mkota,uk. *330*)

86. Mtoto ni kito, mzigo mzito (Mkota,uk. *352*)

87. Mtu pweke ni uvundo (Mkota,uk. *358*)

88. Muungwana ni kamba, hufa na uwao (Mkota, uk. *366)*

89. Ghofira ni ondoleo la dhambi (Mkota,Uk.(131)

90. Jaha ni majaliwa (Mkota,uk. *162*)

91. Ugeni ni utoto (Mkota, uk. *486*

92. Uwongo ni mbio ya sakafuni (Mkota,uk. *532*

93. Zana za vita ni silaha (Mkota,uk. *556*

94. Zinguo la mtukutu ni ufito (Mkota,uk. *557*

95. Damu ni damu si kitarasa (Mkota, uk. *100*)

96. Dalili ya ushehe ni kilemba (Mkota, uk. *101*)

97. Dawa ya moto ni moto (Mkota, uk. *327*

98. Umasikini ni ngozi (Kingei na Ndalu methali, *2249*)

99. Umoja ni nguvu, utengano ni udhahifu (Kingei na Ndalu, methaali, *2265*)

100. Usiku ni libasi bora (Kingei na Ndalu,methali *2312*)

101. Asante ya punda ni mateke (Mkota,uk. 45)

**SITIARI FUNGE**

102. Akili ni taa, miangaza yake mbalimbali (Mkota,uk. 19)

103. Buibui ni mke, mme wajifanyaje (Kingei & Ndalu; methali 277)

104. Maisha ni mbe, hapana kilichomo (Kingei & Ndalu; methali 1030)

105. Maisha ni mlima, kuna kupanda na kushuka (Kingei & Ndalu; methali 1032)

**106. Mgeni ni kuku mweupe (Kingei & Ndalu; methali 1249)**

107. Arukuzuje ni mungu, kiumbe arukuzuni? Mkota,uk. 44

**108. Maisha ni mshumaa uso mkesha (Kingei & Ndalu; methali 1033)**

109. Binadamu ni ngamba, hakosi la kuamba (Mkota, uk. 78

110. Kitendo ni mtoto, majuto ni mjuk.uu huja kinyume. (Kingei & Ndalu; methali 815)

111. Kulima ni bangu, kazi ni ngumu, yataka mwengwangu wa kwenda na kuja. (Kingei & Ndalu; methali 901)

112. Kujidai ni maji ya maharagwe (Mkota,uk. 224)

113. Mali ni kama mvua, inapiga tena inakwenda. (Kingei & Ndalu; methali *1076*)

114. Maneno ni kama fumo, yakitoka mdomoni hajarudi. (Kingei & Ndalu; Methali *1109*)

115. Maneno ni daraja, hajazuii maji kuteremka (Kingei & Ndalu; Methali *1117*)

116. Mapenzi ni majani, popote penye mbolea huchipuka. (Kingei & Ndalu; Methali *1118*)

117. Mjinga ni mtu, usambe ngombe (Kingei & Ndalu; methali *1279*)

**118. Mke ni nguo, mgomba ni kupalilia (Kingei & Ndalu; methali *1306*)**

119. Sheria ni msumeno, uk.ata mbele na nyuma (Kingei & Ndalu; methali *1985*)

120. Undugu ni kovu, hafutiki (Kingei & Ndalu; *2121*)

121. Ugambi ni wa wenye ndumba (Kingei & Ndalu; methali *2127*)

122. Ugonjwa ni suna, kufa ni faradhi (Kingei & Ndalu; methali *2129*)

123. Ujana ni moshi uendapo haurudi (Kingei & Ndalu; methali *2132*)

124. Ujana ni tembo la nazi, halikawii kupita (Kingei & Ndalu; methali *2136*)

125. Ujasiri wa mjinga ni mleli wa tausi (Kingei & Ndalu; methali *2141*)

**126. Ujiraji ni fedha katika kasha (Kingei na Ndalu: methali 2146)**

127. Ulimwengu ni ngwe mbovu, mtu hajitetei nao (Kingei & Ndalu; Methali *2241*)

128. Utajiri ni umande, hutanda na kuyeyuka (Kingei & Ndalu; methali *2363*)

129. Utajiri ni raha ya leo duniani, mateso ya kesho ahera. (Kingei & Ndalu; methali *2362*)